SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 253,545,950
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

## NORWAY kujenga hospitali kubwa ya moyo Zanzibar



ama
ALHAMISI JUNI 16, 2022
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 13
Jinsi wana- misitu Mwanza watetea hoja mbadala gesi haina pingamizi

Maisha mapya Hospitali ya Rufani Mwananyamala sasa iki'ngara upya
Ukurasa 14

UNAUJUA UGONJWA LUPUS?
Anayeugua asimulia mazito yake, gharama na upekee usio kawaida
• Leo mzee, akumbuka mazito kila umri
• Awa kitendawili Muhimbili, nje ya nchi

Na Flora Wingia

LUPUS ni ugonjwa ulioko katika sehemu mbalimbali duniani, lakini kwa Tanzania haufahamiki sana. Wagonjwa wapo waugua kimya kimya hadi hivi karibuni, baadhi yao waliamua kupaza sauti ya kupatiwa msaada wa tiba.

Ni ugonjwa sugu unaohusu mfumo wa kinga mwilini kushambuliwa kwa mtindo na kuwa na kipindi cha kupata nafuu kama vile amepona na kisha inamshambulia sana mtu akawa hoi kiafya.

Waathirika zaidi ni wanawake wanaofika wastani wa asilimia 90 ya wagonjwa, mara nyingi kuanzia umri wa kubeba ujauzito.

Mtaalamu Erik Stratman kutoka kliniki ya Marshfield anafafanua kuwapo dalili kuu tatu zinazomshambulia sana mgonjwa kila kiungo; homa, maumivu ya viungo na vipele.

Pia, anataja kuwapo dalili za uchovu mwilini, kupungua uzito, figo kushindwa kufanya kazi, mapafu yanajaa maji, degedege, shinikizo la mapafu, maumivu tumbo, kichefuchefu, upungufu wa damu, chembe mwilini.

Ni shida ya afya vipimo vyake vinajumuisha hali ya vinasaba (DNA), kinga mwilini, wingi wa damu, chembe chembe sahani, uwezo wa figo na maini yanavyofanya kazi.

Kimsingi, watalaamu wanasema hakuna kinga zaidi ya kutibu dalili na kupunguza makali, huku matibabu yanagusa dawa kama za malaria, pia za kuzuia maumivu.

Namna ugonjwa Lupus unavyoshambulia katika mwili wa mtu. PICHA: MTANDAO.

MGONJWA AJIELEZA

Wiki hii, Nipashe ilizungumza na mgonjwa mmojawapo, akisimulia dalili kama anazopitia, ili ikiwasibu wengine watafute msaada wa matibabu mapema.

Stella Leonard (60), mkazi wa jijini Dar es Salaam, anaelezea hatua zake, jinsi ugonjwa ulivyomuanzia hadi alikofika sasa. Je, ni yepi amepitia na changamoto gani alizokumbana nazo katika kujiuguza hadi sasa?

Mama huyo anasimulia: "Tangu nikiwa mdogo umri wa miaka minane, nilikuwa kila siku naumwa mafindofindo kooni (tonsils), pia mafua ya kila siku na kupiga chafya mara kwa mara. Kwa hiyo, nimekuwa na hiyo historia ya aleji (uzio) hadi nikiwa na umri wa miaka 13, hali ilipokuwa mbaya zaidi.'

Anasema, alipoenda kutibiwa katika Hospitali ya KCMC iliyoko mjini Moshi, Kilimanjaro wakashauri afanyiwe operesheni kuyatoa hayo mafindofindo kooni, hatua iliyotekelezwa.

Stella anasimulia baada ya kupita kipindi ambacho hakumbuki sawasawa, kati ya mwaka mmoja na miwili, madaktari wakagundua tena vitu mithili ya nyama puani, navyo vikatolewa.

Anasema, baada ya hapo aliyojihisi kooni na puani ni kuna uwazi, hata akaanza kupata adha ya kila kitu akihisi kibaya, mfano vumbi linamuingia kirahisi.

"Nikawa nateseka sana kwa kuumwa, hivyo nikaandaliwa utaratibu kupelekwa Nairobi, Kenya kufanyiwa 'allegy Test', kipimo ambacho hapa nchini kilikuwa hakipo miaka hiyo ya 1980," anaeleza mama huyo, akitaja hatua hiyo ilimkuta katika umri wa usichana miaka 23.

Anakiri kutaabika sana na hilo, akiwa na ufafanuzi: "Wakati natolewa mafindofindo kooni, nilikuwa kwenye mafunzo Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makutopora na baadaye nikahamishiwa kambi ya JKT Oljoro. Wakati huo nikawa naumwa tu maafande hawanielewi, nyumbani hawanielewi, nikawa nachoka kila siku nina homa.

"Mwaka 1982 nikapelekwa hospitali moja jijini Nairobi inayoitwa MATA (MATA Miscondect Hospital). Nikafanyiwa hicho kipimo cha aleji na kunitajia vitu ambavyo

Inaendelea Uk. 12

UKURASA 11

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Alhamisi Juni 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580978
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## Utouh apigia makofi alichowasilisha Mwigulu

UKURASA 4

# Serikali yafunguka kodi umri miaka 18

UKURASA 2



"Niseme kuwa nimefurahi sana na jana nimekunywa divai kusherehekea bajeti hii"

LUDOVICK UTOUH



"Bajeti hiyo imeendana na rasilimali zilizopo na hali ya uchumi wa kidunia na kama ikitekelezwa ipasavyo, italeta maendeleo katika nchi."

PROF. RAZACK LOKINA



"Bajeti inayopendekezwa inaashiria serikali imedhamiria kubana matumizi na ubadhirifu."

DK. DONATH OLOMI



"Ni muhimu serikali kupunguza tozo zilizopo kwenye mafuta kuliko kuweka ruzuku kwa kuwa ni sawa na kuchukua fedha mfuko huu na kuweka mfuko wa pili."

DK. CHARLES KIMEI




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wapili kulia), akipokea mfano wa hundi yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 30.7 kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati), jijini Dodoma jana, ambazo ni gawio kwa serikali. Wengine ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Dk. Edwin Mhede (wapili kushoto) na Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 8

## MBARONI TUHUMA KUPANGA MAUAJI DHIDI YA MLALAMIKAJI

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kudaiwa kula njama za kutaka kumuua Kelvin Izack. Akizungumzia tukio hilo jana...

## Chongolo aonya majina ya vigogo uchaguzi CCM

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA REKODI NYUMBANI, YANGA MECHI ZA UGENINI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza na viongozi wa dini wa kitaifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Dini, Askofu Mkuu wa Kanisa la Menonite, Nelson Kisare (kulia kwake), ofisini kwake bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Serikali yafunguka kodi umri miaka 18

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imefafanua uamuzi wake wa kutoza kodi kwa kila Mtanzania aliyefikisha miaka 18, kuwa ni kuongoza wigo wa mlipaji kodi kutokana na walipaji kuwa wachache licha ya wazalishaji kuwa wengi.

Hata hivyo, Naibu Spika Mussa Zungu, amesema Wizara ya Fedha sio sikivu kwa kuwa mara kadhaa imeshauriwa namna ya kuongeza wigo wa kodi, lakini haijapokea kwa utekelezaji.

Wakizungumza wakati wabunge wakijadili mjadala wa hali ya uchumi mwaka 2021, mpango wa taifa na bajeti ya serikali, kwa jicho la wataalamu na watafiti mbalimbali, Kamishna wa Idara ya Sera, Wizara ya Fedha na Mipango, Elihaj Mwandumbya, alisema Sheria ya Kodi ya Mapato inatoa wajibu kwa kila mwenye mapato zaidi ya Shilingi milioni nne, kulipa kodi.

"Ikiwa mwananchi ana mapato chini ya shilingi milioni nne, halipi kodi ya mapato, utawajua kwa miamala inayoendelea kufanyika katika shughuli za uchumi za kila siku, mfano kilimo, biashara, lengo letu ni kumkaribia kila mmoja ambaye mapato yake yanazidi kiwango hicho na turahisishe kwa kutumia TEHAMA alipe kodi alipo," alisema.

"Kwa ambaye ana mapato ya Shilingi milioni nne au zaidi, kiwango chake cha kuanzia ni Sh. 100,000 kwa mwaka. Tunawaomba wabunge waelewe hatulengi kumlipisha kodi kila mtu, tunalenga kumpa chachu mwenye kipato na kwa mujibu wa sheria kinapaswa kulipwa kodi na kama yupo nje ya wigo wa kodi alipe kama sheria inavyotaka," alisema.

Alisema Tanzania ina zaidi ya watu milioni 60 na katika familia kila watu wanane kwa kiwango cha chini kuna mtu mmoja ambaye ana kipato kinachopaswa kulipa kodi.

"Tunapaswa kuwa na walipa kodi milioni saba au nane, idadi tuliyonayo wenye namba za utambulisho walipa kodi ni takribani milioni tatu, na ukienda ndani zaidi ukatazama wanaochangia kulipa kodi kila mwezi au kwa wastani wa miezi sita mara moja ni chini ya milioni moja," alisema.

Alifafanua kuwa kodi ya Sh. trilioni 2.3 inachangiwa na kundi la walipa kodi chini ya milioni moja, na kwamba pato la ndani ni mchanganyiko ikiwamo ya uchumi ambao sio rasmi.

"Ili uweze kutoza kodi kwenye kundi hilo ni muhimu kuhakikisha kwamba kila mmoja anaona wajibu au haja ya kushiriki kwenye ulipaji wa kodi," alisema.

Mapendekezo ya bajeti ya serikali yaliyowasilishwa juzi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ni kila Mtanzania mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 na mwenye kipato kulipa kodi.

"Ili kutimiza azma hiyo, serikali inakusudia kutoa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) kwa kila Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 au zaidi. Kwa kuwa utaratibu wa usajili wa namba ya Utambulisho wa Taifa (NIDA), unamtaka kila mwananchi mwenye umri wa miaka 18 au zaidi kujisajili," alisema na kuongeza:

"Napendekeza kuwa wale wote wenye NIDA kwa sasa (wanaofikia milioni 19 nchi nzima), wapatiwe namba ya TIN na itumike kwenye miamala yote inayofanyika katika ununuzi na mauzo yanayofanyika ndani ya nchi. Kila mwenye namba ya mlipakodi atapata makadirio yake kwa njia ya simu na kulipa kodi husika kwa njia ya mtandao," alisema waziri.

Alisema waendesha pikipiki wanatumia NIDA kupata leseni na waipate kwa simu TIN ili walipe kodi.

"Napendekeza wananchi wote wenye namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) wapeleke ritani za kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka mara moja.

"Utaratibu huu utachachua utamaduni wa kulipa kodi miongoni mwa Watanzania na hivyo kuiongezea serikali mapato yatokanayo na sekta ambazo hazichangii kwenye makusanyo ya serikali kwa sasa licha ya kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama vile sekta za mifugo, kilimo, uvuvi na nyinginezo," alisema.

**ZUNGU 'AWAKA'**

Kwa upande wake, Naibu Spika Zungu, alisema "Kamati ya Bajeti na Bunge kwa ujumla imeshauri sana maboresho ya makusanyo ya kodi, lakini mmekuwa wabishi sana, inaonyesha labda ubishi huo unatokana na maneno aliyoyasema waziri kuwa mnapenda kuwa wabishi kwa sababu mnanufaika."

"Waziri kasema jana (juzi) kwamba fedha nyingi za umma zinaingia kwenye mikono ya watu, leo makontena wanapeleka Congo halafu wanarudisha Tanzania yote sababu ya ubishi, tulisema mkipunguza kodi 'compliance' (maafikiano) inakuwa kubwa wengi watalipa kodi ambaye hatalipa tunakufa naye," alisisitiza.

Alisema leo mtu anakwenda Dubai, gari mpya ni Dola 100,000, lakini nyinyi (wizara) magari yenu ni Dola 300,000 hamtaki kushuka hata mtu afanye kitu gani.

"Watu wanalalamika kwasababu tunakosa mapato hatutaki kufunguka, soko ni hili mtu anapitisha vitenge vya aina moja, gharama moja, lakini mmoja anachajiwa 400 na mwingine 200," alisema.

"Fedha zinaingia mifukoni kwasababu mnatengeneza mazingira ya rushwa, sisi tunataka hela iingie kwenye mifuko ya serikali, kwa kweli tukifanikiwa tutaweza kukusanya mapato ya ndani hata trilioni 50, nchi inaumia kwasababu ya watu wachache," alisema Zungu ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilala.

# Wataalamu uchumi wanena lao ruzuku ya mafuta bil. 100/-

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WATAALAMU wa uchumi na utafiti wamesema ruzuku ya Sh. bilioni 100 kila mwezi kwenye mafuta, bado haijaonyesha unafuu kwenye maisha ya watu, isipokuwa wafanyabiashara wa bidhaa hiyo.

Hayo yamo katika hoja za wataalamu walipotathimini Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021, Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022/23 na mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, walipowasilishia wabunge jana kwenye Ukumbi wa Msekwa jijini hapa.

Wasomi hao wameshauri kuchukuliwe hatua, ikiwamo kuhamisha sehemu ya faida ya wauza mafuta, iongezwe kwenye ruzuku, ili kuisaidia nchi kuhimili uchumi hata kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na rasilimali za taifa, na kuwaepusha kubeba mzigo wa ruzuku wasionufaika nao moja kwa moja.

"Jambo kubwa la kuangalia ni faida ya kampuni zinazofanya biashara ya mafuta ambazo zinapata faida kwa kila lita Dola za Marekani Sh. 0.12 (sawa na Sh. 276) wakati Kenya wafanyabiashara wanapata faida ya Dola 0.085 (sawa na Sh. 195.5) kwa kila lita ya petroli," alisema mwanazuoni Dk. Charles Sokile.

Mtaalamu huyo ambaye pia ni Mwakilishi Mkazi wa Oxford Policy Management, alishauri kufumuliwa mfumo wa biashara ya mafuta, anaoufafanua unamnufaisha zaidi mfanyabiashara kwa faida kubwa, huku mlolongo wa kodi uliopo kwenye mauzo anaubeba mwananchi, ambaye hayaoni mabadiliko kwa kina.

Rai yake katika hilo, ni kwamba serikali iangalie namna ya kukutana na wafanyabiashara, ili kupunguza faida wanayopata badala ya nguvu kuelekezwa zaidi kwenye ruzuku itokanayo na kodi ya umma.

Alifafanua: "Wapunguze faida yao ilingane basi hata na Kenya wakati tuna changamoto za mfumuko wa bei, ili kupunguza mzigo. Serikali imebeba mzigo kwa kutoa ruzuku ya Sh. bilioni 100. Kama serikali inatoa, kwanini nao wasipunguze faida yao?"

Dk. Sokile aliorodhesha baadhi ya tozo zilizomo kwenye bei ya mafuta ni zinazohudumia: Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kila lita ya mafuta inayouzwa kwa wastani wa Sh. 2900 kwa jijini Dar es Salaam.

Alisisitiza kwamba uamuzi wa kiserikali unaochukuliwa kuhusu ruzuku, mara zote uwe na kawaida ya kulenga kada za hali ya chini na kawaida nchini, ili wawe wanufaika wa keki ya taifa.

Mtaalamu huyo wa uchumi, alieleza namna mojawapo ya ruzuku inavyopaswa kutumiwa, pia ni kujenga uwiano wa bei ya mafuta ili kusiwapo tofauti kubwa kutoka maeneo yaliyo karibu na vyanzo yanakochukuliwa (mathalani bandarini Dar es Salaam) na mikoa ya pembezono akitoa mfano wa Kigoma.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Jehovaness Aikaeli, aliungana na mtangulizi wake, akisema ruzuku ya mafuta bado ina walakini tatizo hilo ni endelevu, vivyo hivyo mpangilio wa matumizi yake hauna sura ya kunufaisha wananchi wa kawaida.

"Ruzuku ya mafuta itakuja kutupa shida mwisho wa siku, kwa sababu itajengwa matarajio ya kuendelea kuwapo kwake, ruzuku hizi zina changamoto kwa sababu huwezi kujua nani kanufaika," alieleza.

"Nchi za za Afrika zilizoweka ruzuku Nigeria na Ghana zilifanya utafiti na kugundua zinanufaisha matajiri na kuacha wananchi wanaogelea kwenye umaskini.

"Shida yake mmeshaijengea jamii imani kuwa ruzuku ni endelevu, wakati mnaitoa kwa muda, itakuwa changamoto kubwa. Ni muhimu tuseme siyo endelevu na tutafute mbinu mbadala," alisema.

Wabunge wasomi walioshiriki mada hiyo, nao walionyesha shaka yao kwa ruzuku ya mafuta na uhusiano wake kumnufaisha wananchi wa kawaida, huku Mbunge wa Moshi Vijijini, Prof. Patrick Ndakideni, akiwa na maswali: "Tangu imeweka hii fedha tujiulize bei ya bidhaa imeshuka?

"Bei ya kukodisha trekta imeshuka? Mwananchi wa kawaida ananufaikaje? Kipi bora wanufaike wachache sana, tena wafanyabiashara au tuwaangalie wananchi wetu?"

Aliungwa mkono na mtaalamu na mzoefu wa shughuli za benki, Dk, Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, aliyeshauri marekebisho kwamba serikali ipunguze tozo zilizopo kwenye mafuta, kuliko kuweka ruzuku hiyo ya Sh. bilioni 100, akiitafsiri "ni sawa na kuchukua fedha mfuko huu na kuweka mfuko wa pili".

SERIKALI YAFAFANUA

Kamishna Idara ya Sera Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, alisema Sh. bilioni 100 imesaidia bidhaa hiyo isipande zaidi kutokana na bei ya soko duniani.

"Wakati tunafanya uchambuzi bei ya dizeli ambayo tuliipa ruzuku ya Sh. 400 kwa lita moja ilitakiwa mwezi huu bei yake iwe 3,700 maana yake endapo bei zingekuwa kwa kiwango hicho bei za bidhaa zingepanda kwa kiwango kikubwa.

"Faida ambayo mwananchi anaipata ni kuhakikisha bei za bidhaa zilizopo sasa hazipati sababu ya kupanda kutokana na bei za mafuta za sasa, tunatambua kwa muda zimepanda hadi kufikia zilipo," alisema.

Mwandumbya alizungumzia hoja za nauli au bei za bidhaa kushuka licha ya kuwapo ruzuku hiyo, wanalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi ili wananchi waone manufaa.

HABARI KITAIFA

# Chongolo aonya majina ya vigogo uchaguzi CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametoa onyo kwa wagombea wa nafasi mbalimbali ndani ya chama wanaotumia majina ya viongozi wakuu kwamba wametuma kugombea.

Amesema viongozi hao wasibebeshwe wagombea kabla ya muda huku akikemea makatibu wa chama na Jumuiya za CCM ambao wameanza kubebwa na wagombea mifukoni na kuzungushwa kwenye hoteli.

Kiongozi huyo alitoa onyo hilo jana alipofungua kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) kilichofanyika jijini hapo.

"Ni aibu unapokuta mtu mzima anatumia jina la kiongozi wake kwamba 'huyu ndiye amenituma, huyu amenipa fursa, huyu ndio ameniambia nijiandae kuchukua fomu kugombea nafasi'.

"Kiongozi tunayemtaka ni mwenye dhamira ya kutupeleka mbele, tumtathmini kwa sifa zake, tusimtathmini kwa kuwa ni wa mtu fulani, kiongozi wa mtu fulani hana dhamira njema na chama chetu," alionya.

Chongolo alisema kuwa tangu kufunguliwa pazia la uchaguzi ndani ya chama na jumuiya zake Aprili Mosi mwaka huu hadi sasa, uchaguzi wa matawi na shina umefanyika.

"Sasa tunakwenda ngazi ya kata, wilaya joto linazidi kupanda, presha inakuwa kubwa zaidi, mtu kugombea nafasi siyo dhambi na hata mtu kutangaza nia wakati ukifika siyo dhambi lakini kuna mambo ambayo tumeanza kujifunza hayafurahishi wala hayavutii.

"Watu sasa hivi wapo 'busy', tayari wameshajipatia nafasi na mbaya sana viongozi wakuu wameshapewa wagombea wote, mimi nina bahati moja ndiyo mwenye kujua taarifa zote kuhusu chama na kinachoendelea kwenye chama chetu," alisema.

Alieleza kuwa kiongozi anayedhamiria kuwa kiongozi hahitaji kuwa na mguu wa pembeni wa kumsaidia kugombea nafasi.

"Hahitaji kutumia jina la kiongozi mwingine ili afanikiwe, kiongozi anayejiamini anajipima, anaangalia nafasi yake anajitathmini, anachukua fomu kwa vigezo na sifa za kwake na siyo sifa za mwingine.

"Kiongozi mwenye dhamira njema ni yule anayesimama kwa miguu yake, Mungu ametuumba ametupa miguu miwili, wewe unayeongeza mingine minne au sita we mwenzetu una changamoto, hatuhitaji viongozi wa namna hiyo, tunataka viongozi watakaosimama useme 'naam huyu ni kiongozi'.

"Inatia aibu sana mimi ninayepokea taarifa niwanong'oneze, kuna watu humu ndani wameshajitengeneza kuwa wagombea wa nafasi za mwenyekiti, makamu mwenyekiti Bara na Zanzibar, kuna watu wamejitengeneza kuwa wagombea wa katibu mkuu, wengine wa Naibu Katibu Mkuu Bara na Zanzibar.

"Sisi ni viongozi tuliopewa dhamana ya kusimamia katiba, kanuni na miongozo halali ya chama chetu, msitupatie wagombea kabla ya muda," Chongolo alionya.

Alisema wagombea wote watapatikana kwa muda, utaratibu na bila kuangalia sifa za pembeni, bali zitaangaliwa sifa za mgombea.

"Tunaangalia huyu katika chama chetu tukimtuma kutafuta kura za chama chetu ana uwezo huo? Tukimwambia awaunganishe kinamama ana uwezo huo? Sifa zinaendana na hicho kigezo tunachokusudia? Tukitaka aende kutusemea mahali, watu watasema naam huyu katoka UWT?

"Tunataka mtu ambaye mwonekano wake, matendo yake, tembea yake, kuongea kwake kuwazungumzia wenzie, kiongozi wa UWT jumuiya mama, lazima afanane na jumuiya yetu, hatutaki viongozi ambao wao ni mabingwa wa kukopa sifa za wenzao ili wazitumie wao, tunataka kiongozi akisimama tunasema hapa tuna kiongozi," alisema.

Alionya sifa ya jumuiya hiyo isiharibiwe na kuwataka kuchagua viongozi kwa awamu na kwa muda unaotakiwa.

"Leo hii kuna watu wanatembea na wenyeviti mfukoni, mimi mwenyekiti wangu huyu hapa nani kakwambia? Tusijipe majukumu ya Mwenyezi Mungu."

"Ngazi ya taifa tuna viongozi na hatubadilishi, wenyeviti wa mikoa wapo, na wabaraza wa mikoa wapo, ukijipitisha sasa hivi unavunja kanuni na katiba ya chama chetu, na mimi watu wangu nimewaweka macho waendelee kufanya kazi hiyo, hatulali wala hatupoi, mpaka muda ufike.

"Hakuna kazi rahisi kama kukata jina la mtu aliyevunja kanuni, wala huhitaji muda ukikaa peke yako unaangalia huyu, yaani huyu," alisema.

**ONYO KALI**

Katibu Mkuu huyo alisema: "Nitoe onyo kwa makatibu wangu wa jumuiya tangu mmekuja ninaambiwa mnazungushwa hoteli hii mara hii, habari ninazo na bahati mbaya ninajua makatibu wangu wa jumuiya kwa orodha, ushahidi na kila kitu mnazungushwa kutoka hoteli moja kwenda nyingine leo mpo Kibo, kesho Dodoma hoteli, keshokutwa Kidia."

Alisisitiza kuwa makatibu hao ni wakurugenzi wa uchaguzi, hivyo hatamani na asingependa wanaingia kwenye ushabiki wa kutafuta na kutengeneza wagombea.

"Makatibu wangu ninajua ninyi mnahama hoteli moja kwenda nyingine, kazi ni nzuri ukiikosa lakini ni mbaya sana ukiwa nayo, ukitaka kujua tafuta aliyekuwa nayo akaikosa na bahati mbaya hao mnaowahangaikia hawana uwezo wa kuwarudisha kwenye nafasi zenu baada ya uchaguzi.

"Acheni kubebana bebana kwenye hoteli mnaaibisha jumuiya yetu na chama, umepewa dhamana ya kuwa mtendaji, kaa kwenye utendaji."

Alisema wanawake wanatatizo moja kwenye suala la kupendana, kusemeana mema na kuwataka kutafuta njia ya kubadilisha na waungane kutafuta viongozi bora ambao watafanya UWT kuendelea kuwa nguzo ya chama.

"Tujenge umoja miongoni mwetu na tusemeane mazuri shida yetu moja wakati huu wa uchaguzi tunapenda kutengeneza uongo, kusingiziana, tuwe wa kweli na tusimamie ukweli wa kuendelea kusimamia jumuiya yetu,"alisema.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudentia Kabaka, alisema baraza hilo ni la mwisho kuelekea kwenye uchaguzi ndani ya jumuiya hiyo na kuwataka watendaji kutojiingiza kuambatana na wagombea.

"Mimi Mwenyekiti pamoja na Katibu Mkuu tutakuwa macho kuhakikisha uchaguzi unakuwa wa amani na za kufuata utaratibu," alisema.


PLASCON
COLOUR YOUR WORLD

## Akzo Nobel N.V yaihodhi Kansai Paint Co. Ltd

Kansai Paint Co. Ltd, wazalishaji wa bidhaa ya "Kansai Paint" wameingia makubaliano ya kuuza kampuni yake tanzu iliyoko barani Afrika kwa kampuni ya Akzo Nobel N.V.

Akzo Nobel N.V ni kampuni kubwa ya uuzaji wa rangi duniani. Mauzo yake yametokana na kukamilika kwa taratibu zote stahiki kutoka katika mamlaka husika na malipo yake yatakamilika mwanzoni mwa mwaka 2023.

Kunishi Moro, ambaye ni Rais wa Kansai Paint, anasema kuwa, "Tumejiridhisha kuwa kampuni ya Akzo Nobel ni kampuni kubwa ya rangi na kwa kuwa bidhaa hiyo ndiyo mhimili wa uendeshaji wa kampuni, tunaamini kupitia bidhaa hiyo itaweza kufungua fursa nyingi za biashara hiyo na baadaye kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi za Kiafrika."

Kampuni hiyo imejijengea historia ya aina yake tangu mwaka 1646 na imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Euronext Amsterdam.

Pia inaelezwa kuwa kampuni inaendesha shughuli zake katika nchi zaidi ya 150, ikiajiri watu takriban 33,000 duniani na kufanya mauzo yanayokadiriwa kufikia Euro 9.6 bilioni (sawa na Yen 1.3 trilioni) mwaka 2021.

Kufuatia Mkakati wake wa "Kukuza na Kuuza" kampuni hiyo imekuwa ikisambaza bidhaa mbalimbali za rangi kwa nchi za Afrika Kusini na Kenya nk.

Wawekezaji hao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika ustawi endelevu wa nchi nyingi za Kiafrika kwa muda mrefu kupitia miradi yake mbalimbali ya maendeleo na bidhaa endelevu sambamba na urudushaji kwa jamii, taasisi ya SOS Children ikiwa mojawapo ya jamii hizo.




**Arvind Shekhawat, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kansai Plascon East Africa**

"Kuhodhi shughuli za kampuni ya Kansai Paint barani Afrika kutatuwezesha kutanua wigo wetu wa biashara ya bidhaa mbalimbali za rangi barani humo na kutuhakikishia fursa ya ukuaji zaidi. Ununuzi wa kampuni hiyo unatafsiri jitihada za dhati za uvumbuzi na uendelevu wa kampuni hiyo, na tuna shauku ya kuchanganya ujuzi wetu, ambao utachagiza kuwa na bidhaa bunifu na masuluhisho endelevu kwa wateja wetu," anaeleza Thierry Vanlacker, Ofisa Mtendaji Mkuu na Mwenyekiti wa Bodi ya Akzo Nobel.

Kwa kampuni ya Kansai Plascon Afrika hususan zile zilizoko katika nchi za Kenya, Tanzania, Uganda, Zanzibar na Burundi makubaliano haya ni fursa ya ukuaji zaidi. Tumekuwa na mafanikio makubwa chini ya uongozi wa Kansai Paint na kuweza kukabili ana na kutokutabirika kwa soko wakati wa janga la Uviko-19. "Tunashukuru kwa msaada wa dhati wa kampuni ya Kansai Paint.

Kuelekea mbele, tunaamini kuwa kampuni ya Akzo Nobel itazipeleka biashara zetu mbali zaidi na kwa kuwa kampuni hiyo inajielekeza katika uwekezaji kwenye usalama, jamii na utawala (ESG) ambapo inajikita katika uvumbuzi, maendeleo ya wafanyakazi, fursa pana za kada hiyo vile vile mafanikio ya muda mrefu ya biashara yake barani Afrika," anasema Arvind Shekhawat, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kansai Plascon East Africa.

Plascon ina uongozi mkubwa wa soko kwa Uganda na ikiwa kiongozi katika Ukanda wa Afrika Mashariki, katika nafasi hiyo, ina fursa kubwa ya kukuza biashara yake kuipeleka katika hadhi ya juu zaidi chini ya uongozi mpya wa Akzo Nobel.

Safari ijayo kulingana na Ofisa huyo itakuwa ni aina yake kwa kuwa kampuni imejipanga kutengeneza mkakati, bidhaa, huduma na chapa zitakazoongeza thamani zaidi katika soko la Afrika Mashariki kwa namna endelevu na kwa utaratibu.

Akizungumzia jambo hilo, Jan-Piet Van Kesteren, Mtendaji Mkuu wa Akzo Nobel barani Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika anasema kuwa, "Hatua ya kuhodhi kampuni ya Kansai Paint Africa una faida kubwa katika biashara yetu iliyojimariisha ikiendeshwa katika nchi tisa barani Afrika.

216903901

# Norway kujenga hospitali kubwa ya moyo Z'bar

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya kisasa ya kutibu maradhi ya moyo, inatarajiwa kujengwa visiwani Zanzibar na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Hauklend kutoka nchini Norway.

Kukamilika kwa ujenzi huo, kutasaidia wagonjwa wa moyo kupatiwa matibabu visiwani humo na kupunguza gharama za kwenda nje ya nchi kufuata matibabu.

Katika taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari na Idara ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, ilieleza kuwa, iliahidi kujenga hospitali hiyo hivi karibuni.

Rais Hussein Ally Mwinyi, akiukaribisha ugeni huo, alieleza kuwa, ujenzi wa hospitali hiyo utasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa huduma za maradhi ya moyo Zanzibar na kupunguza kuwasafirisha wagonjwa kwenda nje ya nchi.

Rais Mwinyi alisema, serikali inathamini uhusiano na ushirikiano kati yake na hospitali hiyo ambao ulianza mwaka 2007.

"Ushirikiano huu umeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya afya Unguja na Pemba ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya hospitali kwa ajili ya kinamama na watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kusaidia ujenzi na vifaa katika Hospitali ya Kidongo Chekundu pamoja na kusaidia vifaa tiba kadhaa," alisema Rais Mwinyi.

Vile vile, alitoa shukurani kwa uongozi wa hospitali hiyo kwa kuendelea kushirikiana, kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuendeleza mafunzo kwa wauguzi na madaktari wazalendo na kubadilishana uzoefu.

Pia, alieleza haja ya kuimarisha mifumo katika sekta ya afya hatua itakayosaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wa uongozi wa hospitali hiyo, ulimweleza Rais Mwinyi kuwa lengo la kujenga hospitali hiyo ni kutoa huduma za maradhi ya moyo kisiwani humo.

Uongozi huo ulimhakikishia Rais Mwinyi kwamba wako tayari kuanza ujenzi huo ndani ya mwaka huu kwa sababu wameshajipanga kuanza mradi huo mkubwa.

Kadhalika, uongozi huo ulisisitiza hatua hiyo ni miongoni mwa juhudi zao wanazoendelea kuzichukua katika kuhakikisha wanaendeleza uhusiano na ushirikano uliopo ambao ulianzishwa maalum kwa lengo la kuimarisha sekta ya afya hapa Zanzibar.

Rais Mwinyi alikutana pia na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi chenye Usawa (GEF), ikiongozwa na mwenyekiti wake, Angellah Kairuki, na aliihakikishia kamati hiyo kwamba serikali itaufikisha Mpango wa Utekelezaji wa Kamati hiyo katika Baraza la Mapinduzi ili serikali iuelewe kwa undani zaidi na kuufanyia kazi.

Alieleza kufurahishwa na utaratibu wa kupata matokeo yanayotarajiwa kwa sababu ni njia nzuri ya kupata matokeo yanayotarajiwa na pia ni njia nzuri za kufanya tathmini.

Awali, mwenyekiti wa kamati hiyo, aliitambulisha kamati pamoja na kumjulisha Rais Mwinyi jitihada zilizofanyika tangu kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Desemba 16, 2021 jijini Dodoma.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiagana na Kiongozi wa Ujumbe wa Wafadhili kutoka Chuo Kikuu cha Hauklend cha nchini Norway, Trond Mohn, baada ya kumaliza mazungumzo yao, Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

Alisema kuwa, katika kuhakikisha utekelezaji wa ahadi za nchi, kamati hiyo ya ushauri ya kitaifa yenye wajumbe 25 kutoka serikalini na Asasi za Kiraia, taasisi za elimu ya juu, taasisi za utafiti na sekta binafsi na wajumbe 19 kutoka Tanzania Bara na sita kutoka Zanzibar imeundwa ili kushauri jinsi ya kuhakikisha ahadi za nchi zinafikiwa.

# Utouh apigia makofi alichowasilisha Mwigulu

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya serikali kuwasilisha bungeni mapendekezo ya makadirio na mapato na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2022/23, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, ameyapongeza kuwa ni mazuri yanayolenga kupanua wigo mpana wa ulipaji kodi.

Akizungumza na Nipashe jana, Utouh alisema serikali imesema kila aliye na umri unaoanzia miaka 18 na kuendelea atapaswa kuwa na Namba ya Mlipakodi (TIN).

"Ukiwa na TIN maana yake unatakiwa kulipa kodi. Hiki ni kitu ambacho ukienda Kenya kinatumika, ukisikiliza bajeti hii muhimu sana ni pale Waziri (Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba) alipoongelea suala la Mkaguzi wa Ndani na umuhimu wa kupata fungu ili impe uhuru wa utendaji kazi zake.

"Kama utakumbuka wakati Rais (Samia Suluhu Hassan) anapokea ripoti ya CAG Machi 30, mwaka huu, alizungumzia na kushauri kwamba mfumo mzima wa ukaguzi wa ndani uangaliwe.

"Jana (juzi) waziri alisema Mkaguzi wa Ndani apewe fungu na serikali inaangalia mfumo mzima wa yeye aweze kuwa na matokeo chanya zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Hili ni suala ambalo Taasisi ya WAJIBU tulikuwa tunalitetea," alisema.

Utouh ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alisema wanaamini CAG akipewa mamlaka, rasilimali watu na uhuru wa kufanya kazi zake bila kuingiliwa, 'madudu' mengi ambayo wameyaona kwenye ripoti yake mwaka huu, yanaweza kupungua kwa nusu yake au zaidi ya hapo.

Alisema tatizo moja kubwa ambalo 'ma-CAG' wote duniani hukutana nalo ni 'ile unaangalia kitu na unakiona kina athari kubwa kwa serikali, unatoa pendekezo kifanyike nini ili isitokee, halafu hakuna anayechukua hiyo tahadhari'.

"Tatizo kubwa ni kutokuwapo na kasi ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na mapendekezo yanayotokana na zile kamati za usimamizi za Bunge.

"Bunge linaishauri serikali, ushauri unabaki kuwa ushauri, ni yenyewe serikali kuamua kutekeleza, ninafikiri ipo haja kubwa ya kuona kwamba mapendekezo yanayotolewa na CAG na yakaja yakasisitizwa na Bunge kupitia kamati zake za kudumu za uongozi, serikali ingetafuta utaratibu wa kuyashughulikia.

"Inaposhindwa kuyashughulikia kwa sababu ripoti za CAG ni ripoti za umma, basi iambie umma. Hili tumelishindwa kwa sababu hizi, lakini kutokufanya inakinzana na uwajibikaji ambayo sisi WAJIBU ndiyo tunaoongoza hili," alisema.

Kuhusu Deni la Taifa, Utouh alisema kwa vigezo vya mashirika ya kimataifa ya dunia, bado lipo himilivu lakini wamekuwa wakiishauri serikali wakati ikiendelea kukopa iwe na ubunifu wa kutafuta vyanzo vipya vya mapato.

Alisema kwa bajeti hiyo pendekezwa, kama kila aliye na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea atawajibika kulipa kodi, ikifanyika vizuri itachangia kuongeza mapato ya serikali na hivyo kupunguza mzigo wa Deni la Taifa.

"Niseme kuwa nimefurahi sana na jana nimekunywa divai kusherehekea bajeti hii kwa sababu wakati mwingine utaratibu wa uendeshaji wa serikali unakuwa ni sababu yenyewe ya kuongeza gharama za uendeshaji wa serikali.

"Ninashukuru hili suala lilianza kuzungumzwa tangu bungeni kuhusu madereva wanakaa kwenye magari na kiyoyozi kikiwa kimewashwa kuanzia saa mbili mpaka saa sita usiku ni matumizi makubwa ya petroli, fikiria hali ya petroli kwa sasa ilivyo kubwa, ile kwamba serikali imekemea kwa kusema huo utaratibu usitishwe mara moja, ni kitu kizuri sana."

Alisema haoni ni kwa nini ofisa atoke Dar es Salaam apande ndege kwenda Mwanza halafu gari litoke Dar es Salaam kumfuata aliko.

"Kule Mwanza kama ni usafiri kuna teksi, Bolt, UBA, Watanzania na nafasi zetu nyingi tujifunze kubana matumizi, huko nyuma ilikuwa hili haliumi lakini ukiangalia gharama za kusafiri kwa ndege, gharama za gari kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma hadi Mwanza, gharama yake inakuwa ni mara mbili, huu ni mzigo kwa serikali," alisema.

Utouh alisema eneo lingine ambalo serikali imebana matumizi ni lile la kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari, utaratibu ambao alisema Rwanda inautumia.

Alisema kwa kufanya hivyo kutakuwa na kubana matumizi makubwa ya gharama za uendeshaji wa serikali.

HABARI KITAIFA

# Wachumi waona nuru katika bajeti ya serikali

**Na Jenifer Gilla**

WACHUMI wametoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yaliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma juzi.

Akiwakilisha mapendekezo hayo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.48 katika mwaka huo wa fedha.

Meneja wa Fedha na Utawala wa Taasisi ya WAJIBU, Jackson Mmari, akizungumza na Nipashe jana, alisema bajeti pendekezwa imeonyesha nia ya serikali kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali na kuhakikisha zilizopo hata kama ni kidogo, zinatumika vizuri.

"Utaona kwamba imeonyesha namna ya kupunguza matumizi. Kwa mfano, kupunguza matumizi ya mafuta kwenye magari ya serikali, kupunguza vikao, hiyo yote ni katika kupunguza gharama zinazoweza kuepukika," alisema.

Mmari alisema serikali pia kupitia bajeti hiyo imeonyesha nia ya kuchochea uwajibikaji kwa kumpa nguvu Mkaguzi wa Ndani kuijenga taasisi anayoiongoza kimifumo, rasilimali na zana atakazozitumia katika kufanya kazi.

"Kwa hiyo, tunatarajia sasa huyo Mkaguzi wa Ndani atakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi wa matumizi yanayofanyika na kudhibiti rushwa na wizi unaotokea," alisema.

Mmary mwenye kiwango cha CPA katika uhasibu, alisema kitendo cha bajeti hiyo kuzingatia suala la uwazi, kitasaidia kupunguza rushwa ikiwamo watumishi wa ngazi za juu hasa wakurugenzi kupatikana kwa kuajiriwa na kuwa njia hiyo italeta viongozi wenye uwezo wa kutosha kufanya kazi.

Mchumi Prof. Razack Lokina, alisema bajeti hiyo imeendana na rasilimali zilizopo na hali ya uchumi wa kidunia na kama ikitekelezwa ipasavyo italeta maendeleo katika nchi.

Alisema kuwa bajeti hiyo imewalenga watu wa chini kutokana na mapendekezo ya kuendeleza miradi ya kimkakati na ujenzi wa miundombinu ikiwamo barabara.

"Bado inalenga kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ilikuwa imeanza na bado wameongeza kujenga barabara kwa hiyo inazidi kupanua soko kwa sababu itasaidia wakulima na wafanyabiashara kufika sokoni,"alisema.

Dk. Charles Sokile, Mkurugenzi Mkazi wa Taasisi ya Utafiti na Sera za Uchumi (Oxford Policy Management), alisema kupitia bajeti hiyo, serikali imeonyesha hatua itakazochukua kwa ajili ya kuhamasisha ukuaji wa uchumi na kukabiliana na changamoto zilizopo ikiwamo mfumko wa bei, uzalishaji unaoshuka na kushuka kwa uchumi duniani.

Alisema pamoja na mazuri hayo, serikali inapaswa kutilia mkazo kwenye mambo makuu manne ikiwamo athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaonekana kuathiri kilimo na kutishia nchi kuingia kwenye njaa.

"Hali ya hewa mwaka huu imekuwa mbaya na mavuno yametoka kidogo kwa hivyo bei ya vyakula inaweza kupanda na kusababisha mfumuko wa bei," alisema.

Kingine alitaja kuwa ni vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vinaathiri bei ya mafuta na vyakula, kushuka kwa uchumi wa dunia kiujumla na matumizi makubwa ya serikali.

"Kwa hiyo, inabidi serikali ivisimamie vitu hivyo vizuri mwaka huu kuliko miaka yote kwa sababu tupo katika kipindi cha kushuka kwa uchumi.

"Kuna baadhi ya maeneo serikali imefanya vizuri ikiwamo kupunguza kodi kwenye baadhi ya maeneo ikiwamo mafuta ghafi ya chakula na vifaa vya kilimo, kwa hilo ninaipongeza sana," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema bajeti inayopendekezwa inaashiria serikali imedhamiria kubana matumizi na ubadhirifu.

Hata hivyo, Dk. Olomi alishauri kuwa katika kuchagua watu wa kuongoza mashirika ya umma, serikali inapaswa kuangalia jinsi taasisi zenye mtaji wa serikali zinavyofanya kazi na kuweka mazingira mazuri ya ukuaji wa sekta binafsi.

"Ili kupata kupata viongozi bora katika taasisi, tunahitaji kuunda tume maalum itakayoongozwa na sheria itakayojumuisha wataalamu ambao watasaidia kuhakiki watu wanaofaa," alishauri.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, Ng'wilabuzu Ludigija (watatu kulia), akiwa ameshika keki, wakati Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (kushoto), akimlisha keki hiyo mtoto Arban Ally, anayeishi kwenye mazingira magumu, baada ya kuzindua kampeni ya kata kitaa inayoendeshwa na Pink Tie, jijini humo juzi. Kulia ni Mratibu Dawati la Watoto Wanaoishi Kufanya Kazi Mtaani, Lilian Utillo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majambazi wapora fedha na kujeruhi

**Na Said Hamdani,** LINDI

DIWANI wa Navanga, Tarafa ya Sudi, Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi, Rashidi Mkuya (45), amelazwa katika Hospitali ya Mission Ndanda wilayani Masasi mkoani humo, kutokana na majeraha aliyoyapata baada ya kushambuliwa na majambazi waliokuwa wakipora duka la jirani yake.

Taarifa kutoka eneo la tukio zilizothibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, zinabainisha kuwa tukio hilo lilifanywa na majambazi hao Juni 12 mwaka huu majira ya saa tisa usiku.

Kamanda Kitinkwi alisema majambazi hao ambao idadi yao haijafahamika, walifika nyumbani kwa Ahamad Issa wakiwa na pikipiki kisha kuvunja duka na kuiba televisheni moja na fedha taslimu Sh. 960,000.

Alitaja aina ya televisheni hiyo ambayo iliokoloewa na diwani huyo ni Evoli yenye thamani ya Sh. 350,000.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya majambazi hao kuvamia nyumbani kwa mfanyabiashara huyo, Diwani Mkuya alijitokeza kwa lengo la kutoa msaada na kujikuta akishambuliwa kwa kupigwa nondo kifuani na kichwani.

Alisema licha ya shambulio hilo, diwani huyo alifanikiwa kuokoa televisheni iliyokuwa imeporwa na majambazi hao.

Kamanda huyo alisema wanaendelea kuwasaka majambazi hao na kuwataka wananchi kushirikiana na jeshi hilo katika kuwabaini wahalifu hao ili wachukuliwe hatua za kisheria.

# CCM yawapa mbinu wanawake vita vitendo vya ukatili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimekemea kushamiri kwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia nchini na kuwataka wanawake kupinga kwa nguvu matukio hayo.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Christine Mndeme, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza kwenye kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) kilichofanyika jijini.

Alisema haikubaliki kuendelea kutokea matukio ya aina hiyo nchini na kuwataka pale unyanyasaji au ukatili unapotokea wawe wa kwanza kupinga.

"Watoto wetu wanadhalilika wa kike na wa kiume, vijana wetu wanadhalilika, kina mama wanadhalilika sisi tuonyeshe kwa vitendo kupinga ukatili wa kijinsia na udhalilishaji watoto na wanawake, kwa sababu wote wanatuhusu," alisema.

Mndeme aliwaomba kuendelea kuombea amani kwenye familia zao kwa kuwa siku hizi vijana wanauana na chanzo ni mapenzi.

"Ukiuliza chanzo unaambiwa mapenzi, mapenzi, mapenzi, huyo mapenzi ni nani? Tukemee katika familia zetu," alisema.

Wakati huo, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, amesema bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23 imebeba mwelekeo wenye dhamira ya kupunguza matumizi.

Alisema kitendo cha serikali kupeleka fedha nyingi kwenye kilimo kutaleta mapinduzi makubwa kwa kuwa ni sekta ambayo asilimia 80 ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua nzuri kubana matumizi magari ya serikali

**JUZI** wakati Bajeti ya Serikali ya 2022/23 ikiwasilishwa bungeni na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ilitangaza hatua mbalimbali zinazochukuliwa kubana matumizi ikiwamo kupunguza idadi ya magari yanayotumika kusafirisha viongozi.

Hiyo ni kwa kuzingatia waraka wa Rais namba moja wa mwaka 1998 kuhusu hatua za kubana matumizi ya serikali na waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma namba mbili wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kubana matumizi.

Kama wengi walivyoiita ni bajeti iliyoleta kicheko kwa watu walio kwenye vipato cha chini na kuleta maumivu kwa wenye vipato vya juu.

Katika bajeti hiyo baadhi ya kodi zilizokuwa zikiwaumiza watu wa hali ya chini zimeondolewa, lakini kwa wenye uwezo kuongezewa kwenye maeneo mengine yakiwamo ya burudani.

Kwenye maeneo ambayo yameonekana kutumika kwa gharama kubwa, ilielezwa kuwa kwa sasa serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 558.45 kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari, mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo.

Ili kupunguza gharama hizo imeamua itaondoa utaratibu uliozoeleka wa madereva kutumika kusafiri barabarani na viongozi kwa njia ya anga kwa lengo ya kuyakuta magari kwenye mikoa wanayokwenda kutekeleza majukumu yao.

Imebaini katika utafiti wa siri uliofanyika kuwa kwa siku moja magari ya serikali yaliyotoka Dar es Salaam yalikuwa 132 na yaliyokuwa yanakwenda kwenye jiji hilo yakipishana kwenda Dodoma ni 76 na mengine nane yalikuwa yamepinduka hali inayosababisha gharama kubwa kwa upande wa mafuta, matengenezo na hata posho wanazolipwa madereva.

Katika kuokoa gharama hizo ambazo serikali ilikuwa ikipoteza zaidi ya Sh. bilioni 50, sasa itawakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la serikali wawe na magari yao, wafanye matengenezo, wanunue vipuri wenyewe na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu unaofaa.

Hatua hiyo imeelezwa itaokoa zaidi ya Sh. bilioni 500 ambazo zitaelekezwa kwenye ununuzi wa dawa na kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati, na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Utaratibu huo ni wa busara na hata uangalizi wa magari hayo utakuwa mzuri tofauti na anayelitumia bila kujua maumivu ya kulitengeneza linapoharibika.


Mara kwa mara tumekuwa tukishuhudia magari ya serikali yanavyotumika ndivyo sivyo na hata wengine kubebea mizigo ambayo mingine haifai kubebwa kwenye magari hayo.

Uchungu wa kitu unachokigharamia unakufanya ukitumie kwa uangalifu ili kuokoa gharama zitakazotumika kikiharibika.

Utaratibu huu ukitekelezeka kama serikali yenyewe ilivyoeleza itaokoa mabilioni ya fedha ambazo zitakwenda kutumika kwenye mambo muhimu ikiwamo ununuzi wa dawa na kuokoa maisha ya wananchi wasio na uwezo wa kujitibu.

Vilio vya wananchi kila siku ni ukosefu wa dawa muhimu hospitali, kukosekana kwa majisafi na salama katika baadhi ya maeneo na huduma nyingine zinazogusa maisha ya wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tusijisahau sana, UVIKO-19 bado unarindima kwenye mitaa yetu

TANZANIA iko hatarini kukumbwa na wimbi la tano la ugonjwa wa UVIKO-19. Kutokana na hali hiyo, wananchi wanaaswa kuchukua tahadhari zote zinazoelekezwa na wataalamu wa afya, ikiwamo kupata chanjo stahiki.

Nikisimamia taarifa kwa umma ya mwenendo wa ugonjwa huo nchini, iliyotolewa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika kipindi kama cha mwezi mmoja kuanzia Mei 5 hadi Juni 3 mwaka huu.

Waziri Ummy anasema katika kipindi hicho jumla ya visa vipya 161, vilithibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19, ikilinganishwa na visa 68 vya kipindi cha Aprili 2 hadi Mei 4, mwaka huu.

Anasema, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 137, na kwamba, katika kipindi cha miezi miwili mfululizo, hakuna kifo kilichoripotiwa na kufafanua kuwa, hali hiyo inaaminisha kuongezeka kwa maambukizi katika jamii.

Nadhani kwamba sentesi hiyo ya waziri isitutishe, kila Mtanzania akijiweka sawa kuchukua hatua sahihi zitakazomwezesha kujikinga na ugonjwa huo.

Hapo kuna kipengele cha kukumbushana kuwa makini na umuhimu wa kwenda mahali husika kupata huduma za chanjo, hata mtu awe katika usalama zaidi.

Mara zote katika utoaji chanjo na kumpatia mtu huduma inayomwezesha huwa salama, mwongozo sahihi unaelekeza uvaaji barakoa kwa usahihi wakati wote unapokuwa kwenye maeneo yenye mikusanyiko au pindi unapojisikia dalili za mafua, ili kuzuia kusambaa kwa maambukizi.

Aidha, unaelekeza pia kuuzingatia usafi binafsi, ikiwamo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono, mara kwa mara na kuwahi katika vituo vya afya endapo utakuwa na dalili za ugonjwa huo.

Kuna mkazo unamuwia mtu kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili imara, kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora, kutoa taarifa za kuwapo watu wenye dalili za ugonjwa huo katika jamii kupitia namba ya simu ya bure 199.

**Mara zote katika utoaji chanjo na kumpatia mtu huduma inayomwezesha huwa salama, mwongozo sahihi unaelekeza uvaaji barakoa kwa usahihi wakati wote unapokuwa kwenye maeneo yenye mikusanyiko au pindi unapojisikia dalili za mafua, ili kuzuia kusambaa kwa maambukizi.**

Pamoja na kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya, ni vyema pia kukaongezewa kasi ya utoaji elimu na uhamasishaji jamii kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, ili kuendelea kuwa mahali salama zaidi.

Elimu na uhamasishaji vinahitajika, kwa sababu suala la chanjo liliingiliwa na wataalamu wa mitaani ambao nao wamekuwa wakielimisha jamii kinyume na kile kinachofanywa na wataalamu wa afya.

Mchanganuo wa waliothibitika katika kipindi cha Mei 5 hadi Juni 3, mwaka huu, unaonyesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam uliripoti matukio 130; Arusha 10; Mwanza watano; Shinyanga wanne; Mtwara watatu; na Dodoma na Morogoro ni wawili kila moja.

Pia mikoa ya Morogoro, Simiyu, Katavi, Kilimanjaro, na Mbeya ikawa na mikasa mmoja kila mkoa, huku wagonjwa watatu waliothibitika kuwa na UVIKO-19 waliolazwa, wote walikuwa hawajapata chanjo.

Takwimu zinaonyesha kwamba, chanjo ni kinga dhidi ya madhara ya UVIKO-19, basi ni vyema kila Mtanzania awe tayari kuchukua hatua sahihi zitakazomwezesha kuwa salama zaidi.

Serikali inaendelea kutoa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini, kwa lengo la kuwezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo, kuanzia Mei hadi mwanzo wa Juni, watu 775,680 walipata dozi kamili.

# Serikali kulipa trilioni 2/- PSSSF, NSSF na NHIF

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2022/23, inatarajia kulipa zaidi ya Sh. trilioni 2.67 zilizokopwa kwenye mifuko ya Hifadhi za Jamii ya PSSSF, NSSF na NHIF ikiwamo michango ya wastaafu waliokuwa watumishi kabla ya mwaka 1999.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, aliliambia hayo Bunge jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee.

Mbunge huyo alitaka kujua mpaka sasa serikali inadaiwa kiasi gani cha fedha ambazo imekopa kutoka mifuko hiyo na ni kiasi gani cha madeni kimeshalipwa, pia utaratibu uliotumika.

Naibu Waziri Chande alisema serikali ilikopa fedha kutoka katika mifuko ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na deni la michango ya wastaafu waliokuwa katika utumishi kabla ya mwaka 1999.

Alibainisha kuwa mfuko wa PSSSF zilikopwa Sh. bilioni 506.88 na Sh. bilioni 500 zimelipwa kwa utaratibu wa kibajeti.

"Deni la michango ya wastaafu waliokuwa katika utumishi kabla ya mwaka 1999 lilikuwa Sh. trilioni 4.46 na Sh. trilioni 2.17 zimeshalipwa kwa utaratibu wa hatifungani maalum.

"Aidha, kiasi kilichobaki cha deni la mfuko wa PSSSF, Sh. bilioni 6.88 na Sh. trilioni 2.29 zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/23," alisema.

Alifafanua kuwa mfuko wa NSSF Sh. bilioni 292.59 zilizokidhi vigezo baada ya uhakiki wa deni la Sh. bilioni 490.16 zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/23 huku mfuko wa NHIF, Sh. bilioni 80.68 zilizokidhi vigezo baada ya uhakiki wa deni la Sh. bilioni 209.72, zitalipwa katika bajeti ya mwaka 2022/23.

Naibu waziri huyo alisema serikali itaendelea kuhakiki sehemu iliyobaki ya deni la Mfuko wa NSSF na NHIF ili kujumuishwa katika mpango wa malipo.

# Wataka umoja kuifumua Sheria Huduma Habari

**Na Mary Geofrey**

WAKILI wa kujitegemea amewataka wamiliki wa vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini kuunganisha nguvu na kushirikiana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, katika kufanya mabadiliko ya vifungu vya Sheria za Huduma ya Habari.

James Marenga alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kwenye semina iliyoandaliwa na Jukwaa la Wahariri (TEF) kuhusu maboresho ya sheria hiyo.

Alisema waziri mwenye dhamana ameonyesha nia ya kufanya mabadiliko ya sheria ambazo ni kandamizi hivyo ni wakati wa wadau wa habari kuungana kuendeleza jitihada kuwapo na marekebisho hayo.

"Tumieni majukwaa yenu na vyombo vya habari kueleza changamoto za sheria hizi ili kufanyike maboresho ambayo yataisaidia tasnia ya habari kuendelea kukua," alisema Wakili Marenga.

Kuhusu sheria zenye dosari, wakili huyo alisema zipo zinazosimamia tasnia ya habari ambazo ni mahususi kwa waandishi wa habari.

Alisema sheria hizo zimefanya uandishi wa habari kuwa taaluma rasmi inayotambulika kisheria na imewekwa kwa kanuni mbalimbali za kusimamia.

Wakili Marenga alisema pia imeunda vyombo ikiwamo bodi ya ithibati, kuwapatia waandishi wa habari namba za utambulisho.

Alisema kupitia sheria hiyo kutakuwa na baraza linalosimamia vyombo vya habari na litakuwa linahusika na waandishi wa habari waliopata ujasiri.

Wakili Marenga alisema katika sheria hiyo kuna dosari mbalimbali ambazo zinapigiwa kelele ikiwamo inayompa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO kusimamia usajili wa magazeti kila mwaka.

"Ni changamoto kubwa ambayo waandishi wa habari wanaona inaleta kikwazo kwamba kila mwaka liwe linasajiliwa tofauti na awali, ujasiri ulidumu hadi hapo chombo kitakaposhindwa kufanya shughuli zake," alisema.

Aliongeza kuwa sheria pia imetengeneza makosa ya uchochezi na kashfa na kosa la uchochezi ni tatizo kubwa kwa sababu inabana waandishi wa habari wanaofanya habari za uchunguzi.

"Inasema kuwa endapo mwandishi wa habari ataandika habari ambayo inawafanya wananchi waichukie serikali yao iliyoko madarakani, litakuwa kosa la jinai la uchochezi.

"Ni changamoto kubwa kwa waandishi wa habari kwa sababu wamekuwa wakiandika habari zenye uwiano wa maendeleo kati ya vijijini na mijini ina maana wananchi wakikasirika wakaichukia serikali litakuwa ni kosa.

"Tunaomba sheria hii isiwapo kwa sababu inakinzana na watoa taarifa na wenye haki ya kupata taarifa," Wakili Marenga.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto), akizungumza na Meneja Mkazi wa Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Ltd, Benedict Busunzu, walipokutana jijini Dodoma jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Waziri azungumza na Meneja Tembo Nickel

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekutana na kufanya mazungumzo na Meneja Mkazi wa Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Nickel Tembo Nickel Corporation Ltd, Benedict Busunzu.

Mapema mwaka 202, serikali ilitiliana saini mkataba na Kampuni ya LIZ Nickel ya Uingereza kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya Nickel Kabanga mkoani Kagera pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuchenjulia madini mbalimbali kinachojengwa Kahama, Shinyanga.

Utiaji saini wa mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya LIZ Nickel uliwezesha kuanzishwa kampuni ya pamoja inayoitwa Tembo Nickel Corporation Ltd ambayo ni kampuni ya ubia.

Akizungumza mkoani Dodoma juzi, Meneja Mkazi wa Kampuni ya Tembo Nickel, Busunzu, alimweleza Waziri wa Ardhi kuwa kampuni yake imejipanga vizuri kwa ajili ya kuanza mradi wa uchimbaji madini ya Nickel huko Kabanga, Ngara mkoani Kagera. Alisema hatua ya kwanza waliyochukua ni kuwaelimisha wananchi wanaoishi eneo la mradi ili kuwajengea ufahamu kwa lengo la kuepuka migogoro wakati wa ulipaji fidia kwa wale wananchi watakaohamishwa kupisha mradi.

"Tumetumia muda mrefu kuwaelimisha wananchi kabla ya kuanza uzalishaji wa Nickel hii itatusaidia kuepuka migogoro wakati wa zoezi la ulipaji fidia kwa wale wananchi watakaohamishwa kupisha mradi," alisema Busunzu.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Mabula, alimweleza meneja mkazi huyo kuwa uamuzi wa kutoa elimu kwa wananchi ni nzuri kwa kuwa utasaidia kuepuka migogoro, hasa ile ya fidia kabla ya kuanza mradi.

"Hatua mliyochukua ya kutoa elimu mapema ni nzuri na itasaidia kuondoa migogoro wakati wa zoezi la ulipaji fidia na ni vizuri pia mkafanya utaratibu wa kuthaminisha eneo lote la mradi kama ilivyofanyika kwenye Mgodi wa Nyanzaga kule Sengerema," aliagiza.

Matokeo ya awali ya uzalishaji madini ya Nickel Kabanga wilayani Ngara mkoani Kagera yanaonyesha utakuwa na wastani wa mauzo yenye thamani ya dola za Marekani zaidi ya milioni 664 kwa mwaka.

Katika makubaliano ya mkataba wa mradi huo, serikali itakuwa na umiliki usiopungua asilimia 16 ya hisa za mradi zisizolipiwa na zisizopungua thamani, hivyo kupata gawio kwenye faida zitakazopatikana baada ya kulipa kodi zote stahiki za serikali.

Utafiti uliofanywa na serikali kuanzia mwaka 1976 hadi 1979, ulibaini kuwapo kwa madini ya Nickel katika mwamba unaoanzia eneo la Msongati, Burundi hadi Kabanga na kiwango kikubwa cha Nickel kinapatikana Kabanga ni cha daraja la kwanza.


NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

M/MWANZO YA ILEMELA - SHAURI LA MIRATHI Na. 115/2019

TUMAINI JAMES NDONGO ______ MSIMAMIZI

DHIDI YA

JAMES NDONGO SANGA ______ MAREHEMU

M/MWANZO MWANZA MJINI - SHAURI LA NDOA Na. 07/2017

PLAXEDA MANASE ______ MDAI

DHIDI YA

SAMORA HEBERT ______ MDAIWA

M/MWANZO MKUYUNI – SHAURI LA MADAI Na. 37/2020

REBECA AYUBU ______ MDAI

DHIDI YA

PASCHAL SILVESTER ______ MDAIWA

M/MWANZO SENGEREMA - SHAURI LA MADAI Na. 78/2020

SIYA SAIMONI ______ MDAI

DHIDI YA

JOHN SAIMON ______ MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI, MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI NA MAHAKAMA YA MWANZO SENGEREMA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA NA BOMA LA NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA 3 | NYAMANORO WILAYA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA. | 18/07/2022 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | MTAA WA RUFIJI, WILAYA YA SENGEREMA MKOA WA MWANZA. | 18/07/2022 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | BOMA LA NYUMBA | MTAA WA KUZENZA-NYEGEZI, WILAYA YA NYAMAGANA – MWANZA. | 19/07/2022 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | NYUMBA | IPULI MAHINA WILAYA YA NYAMAGANA MKOA WA MWANZA. | 19/07/2022 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI INAYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

216904902

MAWASILIANO: 0768-588155

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imewahukumu watu watatu kunyongwa mpaka kufa kwa kosa la kumuua January Kasuhuke kwa kumcharanga mapanga mguuni, kichwani na shingoni na kufariki dunia papo hapo.

Washtakiwa hao waliohukumiwa kunyongwa mpaka kufa ni Juma Gulaka (54), Juma Kasanana (53) na Bahati John (50).

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Lilian Itemba, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Jaji Itemba alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia ya kikatili kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na James Pallangyo, ukipeleka mahakamani mashahidi tisa na vielelezo saba ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa walimuua Januari Kasuhuke.

Upande wa Utetezi ulikuwa unaongozwa na mawakili watatu wa kujitegemea ambao ni Laulent Bugoti, Erick Rutehanga na Nestory Kuyula, kila mmoja alimtetea mshtakiwa mmoja.

Jaji Itemba alisema shahidi wa sita alikuwa akipita katika poli la Samina na kusikia kelele za mtu akiomba msaada na alienda sehemu ambapo kelele zilikuwa zikitokea na kushuhudia tukio hilo akiwa umbali wa mita saba akiwa amejificha kichakani.

Alisema alishuhudia tukio hilo kwa muda wa dakika 15, akimwona mshtakiwa wa tatu akimkatakata mapanga marehemu mguuni majira ya saa tano asubuhi katika pori la Samina, Wilaya ya Geita.

Jaji Itemba alisema washtakiwa hao walikodiwa kwa Sh. milioni 2.5 ili kumuua Kasuhuke kwa kuwa alikuwa akifanya mapenzi na mke wa mtu ambaye aliwakodi washtakiwa hao.

Jaji Itemba alisema: "Nimeangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo la mauaji pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama hii inawatia hatiani washtakiwa wote kwa pamoja kwa kosa waliloshtakiwa nalo."

Wakili wa Serikali Winfrida Erenest aliomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria na upande wa utetezi ulidai unaiachia mahakama itoe adhabu.

Jaji Itemba alisema kwa kesi hiyo ya mauaji, mahakama inawahukumu washtakiwa wote kwa pamoja kunyongwa mpaka kufa.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa Februari 3, mwaka 2010, katika eneo la msitu wa Samina, Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walimuua kwa kukusudia January Kasuhuke kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo.




Baadhi ya Wateja wa Benki ya NBC, wakiwa kwenye hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa jijini Mwanza hivi karibuni, ili kujadili fursa za biashara na kutambulisha huduma mpya za benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kupanga mauaji dhidi ya mlalamikaji

**Neema Hussein, KATAVI**

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kudaiwa kula njama za kutaka kumuua Kelvin Izack.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Ibindi Wilaya ya Mpanda mkoani humo.

Kamanda Makame aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Kingi Gabriel (49), Masunga Peter (23) na Simon Fredrick (19), wakazi wa Ibindi.

Alisema chanzo cha kutaka kutekeleza tukio hilo ni wivu wa mapenzi ambapo mlalamikaji Kelvin Izack alimtuhumu mtuhumiwa ambaye ni Kingi Gabriel kuwa anajihusisha kimapenzi na mke wake.

Hata hivyo, Makame alisema mlalamikaji alimwonya mtuhumiwa huo kuacha kufanya mapenzi na mke wake lakini alikaidi na kuendelea kuwa na uhusiano naye. Alisema mtuhumiwa huyo ndipo aliamua kupanga mpango wa kumuua mlalamikaji akiwa na wenzake.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi linatoa rai kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi, akisisitiza kuwa baada ya upelelezi kukamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa taratibu zingine za kisheria.

# Tanzania na China kushirikiana TEHAMA

**Na Frank Monyo**

TANZANIA na China zimekubaliana kuendelea kushirikiana katika kukuza usambazaji wa TEHAMA nchini ili kuhakikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kidijitali inafikiwa.

Makubaliano hayo ya ushirikiano yamefikiwa baina ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian katika mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Nape alisema katika kupeleka huduma za mawasiliano maeneo yasiyofikiwa hasa maeneo ya vijijini, China imekubali kuwa itaendelea kushirikiana na Tanzania ili kuhakikisha lengo hilo linafikiwa.

"Tutaendelea kuwahamasisha wawekezaji wa sekta ya mawasiliano nchini kwetu ili wafikishe huduma za mawasiliano kama ambavyo umeeleza.

"Pamoja na kukubali kwamba suala la usalama mtandaoni linazo changamoto lukuki ambapo China imekuwa ikikabiliana nazo kila uchao, Balozi Mingjian amesisitiza China bado inaona umuhimu wa kushirikiana na Tanzania ili kuhakikisha usalama mtandaoni unakuwa wa uhakika kwa kuweka mazingira na miundombinu itakayowezesha Tanzania kukabili majanga ya kimtandao.

"Kimsingi, tumekubaliana kuboresha zaidi suala la usalama mtandaoni hasa kwenye eneo la capacity building (kujenga uwezo) kwa wataalamu wetu wa TEHAMA, kubadilishana programu za kiteknolojia zitakazowezesha ukuzaji wa sekta mtambuka za maendeleo kiuchumi kwa mfano kilimo, afya, biashara mtandao na kadhalika," alisema.

Katika mkutano huo, pande hizo mbili pia zimekubaliana namna zitakavyowezesha Tanzania kupokea na kukuza teknolojia mpya za mawasiliano ikiwamo teknolojia ya mawasiliano ya kasi ya 5G.

Nape alisema kuwa wizara yake imeendelea kuhakikisha inatekeleza majukumu yake hasa kupitia Idara ya Habari-Maelezo ambapo pande hizo mbili zimekubaliana kuboresha miundombinu ya idara hiyo itakayowezesha kuongeza ufanisi wa utoaji huduma, hasa kwa kuzingatia kuwa idara hiyo inahusika kutoa taarifa mbalimbali za serikali kwa wananchi.

Kuhusu uungwaji mkono katika Ujumbe wa Baraza-Tendaji la Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU), Nape alisema Tanzania mwaka huu inawania kuchaguliwa tena kuingia kwenye baraza hilo katika Mkutano Mkuu wa ITU unaotarajiwa mwezi Septemba baadaye mwaka huu, China imekubali kuwa itaiunga mkono Tanzania, ikitumia fursa hiyo kuomba Tanzania pia iiunge mkono katika nafasi mbalimbali inazowania.

"Balozi Mingjian amesema atafikisha ujumbe pia kwa nchi nyingine rafiki kuiunga mkono Tanzania kuwania nafasi hiyo ambayo itashuhudia nchi 13 za Afrika zikichaguliwa katika nafasi za ITU katika mkutano wa jijini Bucharest nchini Romania utakaoketi Septemba na Oktoba mwaka huu.

"China bado inaona umuhimu wa kushirikiana na Tanzania ili kuhakikisha usalama mtandaoni unakuwa wa uhakika kwa kuweka mazingira na miundombinu itakayowezesha Tanzania kukabili majanga ya kimtandao," alisema.

# Viongozi wa dini wapongeza kupungua vifo vya UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MAKATIBU wakuu wa madhehebu ya dini nchini wameipongeza serikali kwa kupunguza vifo vitokanavyo na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) na kutoa elimu ya matumizi sahihi na endelevu ya dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya Ukimwi (ARV).

Akizungumza juzi kwenye kikao cha makatibu hao kilichofanyika wilayani Morogoro, Charles Kitime, alisema serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) imefanya kazi kubwa ya utoaji wa elimu sahihi na endelevu ya matumizi ya ARV kwa watu wanaoishi na VVU (WAVIU) na vifo vimepungua kwa kiasi kikubwa.

"Elimu hii inayotolewa kwa viongozi wa dini wa kitaifa basi ifikishwe kwa viongozi wa dini wa ngazi ya chini walioko mikoani na wilayani kote nchini kwa kuwa huko ndiko kuna jamii kubwa ambayo pia ina umuhimu wa kupata elimu hii ya kujikinga na maambukizi ya VVU na viongozi hao wanajua lugha sahihi ya kutumia kwa jamii husika," alisema.

Alishauri serikali kuangalia namna nyingine ya kubadilisha mfumo katika vituo vya afya hasa katika huduma za mwitikio wa UKIMWI ili mtu anapokwenda kupata huduma, kusiwe na dirisha maalum kwa ajili ya watu wanaoishi na VVU ili kupunguza unyanyapaa kwa WAVIU.

Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Shekhe Nuhu Mruma, alisisitiza umuhimu wa mafunzo ya uelimishaji namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU kuelekezwa kwa viongozi wa dini wa ngazi ya mkoa.

"Viongozi wa dini ngazi ya chini wapatiwe mafunzo ya uelimishaji namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU kisha wapatiwe vipeperushi pamoja na dhana za kufundishia ili elimu hiyo waitumie kuifikisha kwa walengwa, kule ndipo jamii kubwa iliko," alisema.

Alishauri mpango mkakati wa nchi unaoandaliwa sasa hakikisheni inaangalia namna ya kufikia jamii kubwa kuliko jamii hiyo ambayo ipo juu ikiwa ni pamoja na ujumbe ambao miamvuli ya dini imeshiriki kuandaa lakini hata usambazaji wake uwafikie walengwa, usiishie katika ngazi za juu.

Awali, akiwasilisha maazimio, Mtendaji Mkuu wa Interfaith Platform (TIP), Asna Shendui, alisema imefika wakati sasa wadau wanaofadhili shughuli za UKIMWI nchini kama vile CDC,USAID kuziamini taasisi za dini kuwa na uwezo wa kusimamia fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa taasisi hizo zina mifumo imara kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Jumanne Issango, aliwashukuru viongozi wa dini kwa mchango wao wanaoendelea kuutoa katika jamii.

"TACAIDS itaendelea kushirikiana na majukwaa haya kuendelea kuangalia ni namna gani tunaweza kushirikiana ikiwa ni pamoja na kuzingatia maazimio yenu, tukikaa na wadau wa maendeleo, tutayajadili haya lakini pia hata kwenye mkakati wa tano wa taifa wa kudhibiti UKIMWI hatuwezi kuacha hatua hizi nzuri ambazo tumeishazianza,"alisisitiza Isango.




Wafanyakazi wa Hoteli ya Johari Rotana, Suleiman Nyirenda (kushoto) na Hiyari Mkari, wakitoa damu, hotelini hapo jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuchangia Benki ya Taifa ya Damu Muhimbili. Zaidi ya wafanyakazi 30 wa hoteli hiyo, walichangia damu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CWT yajitosa kuukabili ukatili wa kijinsia nchini

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA cha Walimu (CWT) Mkoa wa Pwani kimeiomba jamii kutoa ushirikiano kwa vyombo vya sheria pale wanapoona kuna viashiria vya ukatili wa kijinsia.

Katibu wa Chama hicho Mkoa wa Pwani, Mwajuma Masenga, amesema taarifa hizo zikitolewa mapema, zitaleta matokeo chanya katika vita vya kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wahusika kudhibitiwa mapema.

Aliyasema hayo juzi kwenye mkutano uliofanyika na lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili walimu wanawake wakiwa kazini.

Mwajuma alisema wanalaani vitendo hivyo ambavyo kwa sasa vinaripotiwa katika maeneo mbalimbali, lakini wanaiasa jamii kuungana kupiga vita vitendo hivyo visiendelee kutokea.

"Hata kwenye maeneo ya kazi tunatakiwa tuzungumze na watoto wasijenge mazoea ya kupokea zawadi kwa kila mtu, hii pia itapunguza vitendo wanavyofanyiwa watoto wetu ambavyo baadhi yao wanaathirika kiafya na wengine kupoteza maisha," alisema.

Mariam Mpunga ambaye ni Katibu wa Wanawake Walimu Mkoa wa Pwani, alisema katika mkutano huo wamejadili mambo mbalimbali ikiwamo kukumbushana suala la maadili kazini.

Mpunga aliendelea kusema walimu wanawake wanao wajibu wa kutetea haki zao wenyewe, lakini kuhakikisha wapambana kwa hali na mali ili kuwalinda wanawake na watoto shuleni na majumbani.

Wajumbe wa Kamati Tendaji CWT Taifa, Herbet Ngimi na Shabani Tesua, walisema walimu pia wanatakiwa kujenga urafiki na wanafunzi na wanapobaini shida watafute namna ya kukabiliana nayo kwa kuwashirikisha wazazi.

Katka mkutano huo Mweka-hazina wa CWT Taifa, Abubakar Alawi, aliwataka walimu kujenga ushirikiano na kuepuka migogoro kazini, pia alichangia kitengo cha wanawake shilingi milioni mbili.

# Kampuni yatoa msaada polisi

**Na John Badi**

KAMPUNI ya Hero Motocorp, watengenezaji wa pikipiki za magurudumu mawili, chini ya kampuni tanzu ya Karimjee Jivanjee Ltd (KJL), imekabidhi msaada wa pikipiki tano za Hero Hunter 125cc kwa Jeshi la Polisi nchini ili kusaidia kuimarisha ulinzi.

Meneja Mkuu wa Karimjee Jivanjee Ltd, William Kadiva, katika hafla ya kukabidhi pikipiki hizo mkoani Dar es Salaam juzi, alisema:

"Karimjee Jivanjee Limited ni biashara ya familia ya karne ya 21 inayoendeshwa na historia na mwongozo wa huduma bora, watu, wateja, washirika, jamii na biashara.

"Karimjee Jivanjee kwa sasa inaendesha shughuli zake katika sekta tano za biashara: Usafiri, Nishati, Huduma za Kifedha, Ukarimu na Mtaji. Tuna chapa nne chini ya mwamvuli wa Karimjee Mobility, Hero Moto corp ikiwa mojawapo ya chapa tanzu.

"Karimjee Mobility ilichukua jukumu la kusambaza pikipiki za Hero mwishoni mwa mwaka 2021 na hadi sasa imefanikiwa kufungua matawi mawili na kuunda mtandao wa wafanyabiashara zaidi ya 20 walioidhinishwa kote Tanzania."

Akitoa maelezo wakati wa uchangiaji huo wa pikipiki kwa polisi, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema: "Pikipiki hizi zitawawezesha askari polisi kuweka ufuatiliaji katika maeneo yao na pia kuimarisha ulinzi kwa ujumla."

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Chang'mbe, Ariziki Mkwaya, aliyepokea pikipiki hizo kwa niaba ya Jeshi la Polisi, alitoa pongezi kwa Meneja Mkuu na kubainisha kuwa msaada huo utasaidia kuwapa motisha askari katika maeneo tofauti.

Alisema William Kadiva, Meneja Mkuu wa KJL, alisema: "Karimjee Group ni wafuasi wa muda mrefu wa vyombo vya sheria na wana historia ya kulisaidia Jeshi la Polisi kupitia chapa zake nyingine mbalimbali.

"Tunatambua sana jukumu la Jeshi la Polisi katika jamii yetu ni kulinda raia na tuna furaha tunaweza kusaidia utekelezaji wa sheria kwa kutumia pikipiki za ubora wa juu za Hero Hunter."

# Mwalimu afariki kwa kuteketea na moto

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Morogoro, Daudi Senyagwa, amefariki dunia baada ya nyumba aliyokuwa akiishi Mtaa wa Seminari, Kata ya Kingoluwira kushika moto na kuteketea.

Mwandishi wa habari hizi alifika eneo la tukio na kushuhudia nyumba hiyo iliyojengwa kwa tofali za saruji, yenye chumba kimoja, choo na sebule, ikiwa imeteketea kwa moto, huku jiko dogo la gesi linalobebana na mtungi wake likionekana pembeni.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo balozi wa nyumba kumi katika eneo hilo, Gregory Tandu, alisema majira ya saa tano usiku alipigiwa simu na jirani yake kuwa kwenye nyumba ya jirani yao kuna moto na alipofika alishuhudia moto na gari ndogo ya mwalimu ikiwa imeegeshwa nje.

"Hakukuwa na dalili ya mtu yeyote kuzunguka eneo hili, tukampigia simu mwenyekiti naye akawapigia simu polisi kuwaarifu, moto ulikuwa mkubwa na kulikuwa na dalili kama ya mlipuko ukitokea kwenye moto," alisema.

Shuhuda mwingine, Abel Palanjo, alisema baada ya kushuhudia moto huo alimpigia simu Tandu afike eneo hilo na kuwajulisha viongozi wengine akiwamo Mwenyekiti wa Mtaa aliyewaarifu Polisi nao kuwaita askari wa Zimamoto na Uokoaji waliofika na kuzima moto huo, ingawa mwalimu aliyekuwa ndani alikuwa ameshapoteza maisha.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Manispaa ya Morogoro, Gaspar Jaka, alisema wamepokea taarifa za tukio hilo kwa masikitiko makubwa ikizingatiwa mwalimu huyo alikuwa muadilifu na mchapakazi.

"Mwalimu alikuwa anafundisha somo la Jiografia Sekondari ya Morogoro, kifo chake kimetutia simanzi kubwa sana na pengo lake sio rahisi kuzibika," alisema Jaka.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Morogoro, Ralph Meela, aliyefika eneo la tukio, alisema taarifa za awali zinaonyesha kifo cha mwalimu huyo kimesababishwa na gesi.

Hata hivyo, alisema wana shaka zaidi na tukio hilo kutokana na kukuta mlango wa nyumba hiyo ukiwa wazi huku funguo wa nyumba ukining'inia kwenye kitasa kwa nje ya mlango.




Soko jipya la Kijiji cha Suguti, Jimbo la Musoma vijijini, mkoani Mara, lililojengwa na serikali ya kijiji hicho, likiwa limekamilika. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kijiji, Sadick Chiguma, soko hilo, litachukua wafanyabiashara wadogo 42 hasa wale wanaofanya shughuli zao kando ya barabara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# H'shauri Namtumbo yapata hati safi

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma imepata hati safi katika matokeo ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ambao ulifanywa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2021.

Akizungumza katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani cha kujadili taarifa ya CAG katika halmashauri hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, aliwapongeza watumishi na Baraza la Madiwani kwa kusahihisha makosa waliyoyafanya mwaka 2019/2020 baada ya kupata hati yenye mashaka.

RC Ibuge alisema hati yenye mashaka katika kipindi hicho ilileta doa kwenye rekodi za kupata hati safi na kwa sasa halmashauri hiyo imerejea kwenye mstari wa kupata hati safi.

"Napenda sasa nitoe maelekezo kama sehemu ya dira katika kujihakikishia kuwa Namtumbo inaendelea kupata hati safi kwa kuhakikisha hoja zote zilizosalia zifungwe, zuieni kujirudia hoja, wakuu wa idara washiriki ipasavyo kuandaa majibu ya hoja na utekelezaji wa mapendekezo ya CAG," alisisitiza Ibuge.

Mkuu wa Mkoa pia ameagiza halmashauri kuchukua mapema hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaozalisha hoja ili isionekane ni jambo la kawaida na upotevu wa mapato katika halmashauri na vyanzo vya upotevu vidhibitiwe ili hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Pia, ameagiza kuwapo umakini katika utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu za manunuzi na kwamba halmashauri iendelee kulipa madeni mbalilmbali ya wazabuni kwa wakati ili iweze kujiendesha kwa tija.

Alipongeza halmashauri hiyo kwa kuchangia asilimia 87.5 mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kuchangia Sh. milioni 83.

Hata hivyo, alisema Halmashauri ya Namtumbo katika mwaka wa fedha 2020/2021, imekusanya mapato ya ndani kwa asilimia 82.62 ya lengo la kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.77 na kufanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.46.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuendelea kuwasimamisha kazi Ofisa Manunuzi, Samson Manjale na Ofisa Maendeleo ya Jamii, Pelesta Mugusha ili kupisha uchunguzi unaoendelea kufanywa na Tume maalum.

Kadhalika, alimuagiza Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, kufanya uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili watumishi hao na kumtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Lucy Kafumu kutoa ushirikiano katika uchunguzi wa TAKUKURU.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ameanza vikao maalum vya Baraza la Madiwani katika halmashauri zote nane ili kujadili taarifa ya CAG.

## Sendiga awataka wananchi kulinda miundombinu TANESCO

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amewataka wananchi kulinda miundombinu ya Shirika la Umeme nchini (TANESCO) ili liendelee kutoa huduma.

Alisema kumekuwapo na tatizo la uharibifu wa miundombinu ya mfumo wa TANESCO inayofanywa na baadhi ya wananchi na kusababisha shirika hilo kushindwa kutoa huduma kwa wakati.

Sendiga alisema hayo jana wakati akizindua huduma mpya ya maombi ya umeme kwa njia ya mtandao (Nikonekt) katika halfa fupi ya uzinduzi iliyofanyika katika viwanja vya ofisi ya TANESCO mkoani hapo.

Aliipongeza TANESCO kwa kuleta mabadiliko chanya katika utoaji huduma na kuongeza kuwa mfumo mpya wa Nikonekt utarahisisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wakati.

Nikonekt ni mfumo rahisi wa maombi ya huduma ya umeme kwa njia ya mtandao (kigitali) ambayo inamwezesha mteja kupata huduma ya mbalimbali bila kufika ofisi za TANESCO.

Aidha, aliwasihi watendaji wa TANESCO kuongeza bidii katika kuwahudumia wananchi.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Sotco Nombo, alisema mfumo huo ni rafiki kwa mteja kwa kuwa anaweza kufanya maombi akiwa popote bila kufika katika ofisi za TANESCO na akaunganishiwa huduma ndani ya siku nne.

Alisema, mfumo huo unatumia njia kuu tatu kufanya kazi; maombi kupitia simu ya kiswaswadu (USSD Code) kwa kupiga namba *152*00# na kwa watumiaji wa simu za kawaida.

"Mteja anaweza kutumia mfumo wa nikonekt kwa kutumia njia ya web portal kupitia www.tanesco.co.tz na pia anaweza kupakua App ya Nikonekt kwenye simu yenye uwezo wa intaneti kupitia Play Store na App Store kwa waumiaji wa iphone."

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Dk. Abel Nyamahanaga, kuendelea kulinda miundombinu ya umeme kwa kutoa taarifa za uharibifu unapotokea ili shirika liendelee kutoa huduma ya umeme.

Alisema kuwa nikonekt ni mfumo mpya na wa kidigitali ambao utakuwa mwarobaini kwa changamoto ya wananchi ya kufuata huduma hiyo katika ofisi za TANESCO, pia utapeli uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wafanyakazi wajulikanao kama vishoka.

Dk. Nyamahanga alisema, kuwapo kwa umeme pia kutasaidia serikali kukusanya mapato ambayo yatatumika kujenga barabara, vituo vya afya, maji, umeme na hospitali.

Steven Mhapa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, alisema kuwa kuwapo kwa mfumo mpya wa maombi ya umeme wa kidigitali kutaondoa usumbufu ambao wananchi kutoka vijijini kwenda ofisi za TANESCO mjini kupanga foleni.

ama
ALHAMISI JUNI 16, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Jinsi wana- misitu Mwanza watetea hoja mbadala gesi haina pingamizi




## Maisha mapya Hospitali ya Rufani Mwananyamala sasa iki'ngara upya

Ukurasa 14

UNAUJUA UGONJWA LUPUS?

# Anayeugua asimulia mazito yake, gharama na upekee usio kawaida

- Leo mzee, akumbuka mazito kila umri
- Awa kitendawili Muhimbili, nje ya nchi

**Na Flora Wingia**

LUPUS ni ugonjwa ulioko katika sehemu mbalimbali duniani, lakini kwa Tanzania haufahamiki sana. Wagonjwa wapo waugua kimya kimya hadi hivi karibuni, baadhi yao waliamua kupaza sauti ya kupatiwa msaada wa tiba.

Ni ugonjwa sugu unaohusu mfumo wa kinga mwilini kushambuliwa kwa mtindo na kuwa na kipindi cha kupata nafuu kama vile amepona na kisha inamshambulia sana mtu akawa hoi kiafya.

Waathirika zaidi ni wanawake wanaofika wastani wa asilimia 90 ya wagonjwa, mara nyingi kuanzia umri wa kubeba ujauzito.

Mtaalamu Erik Stratman kutoka kliniki ya Marshfield anafafanua kuwapo dalili kuu tatu zinazomshambulia sana mgonjwa kila kiungo; homa, maumivu ya viungo na vipele.

Pia, anataja kuwapo dalili za uchovu mwilini, kupungua uzito, figo kushindwa kufanya kazi, mapafu yanajaa maji, degedege, shinikizo la mapafu, maumivu tumbo, kichefuchefu, upungufu wa damu, chembe mwilini.

Ni shida ya afya vipimo vyake vinajumuisha hali ya vinasaba (DNA), kinga mwilini, wingi wa damu, chembe chembe sahani, uwezo wa figo na maini yanavyofanya kazi.



Namna ugonjwa Lupus unavyoshambulia katika mwili wa mtu. **PICHA: MTANDAO.**

Kimsingi, watalaamu wanasema hakuna kinga zaidi ya kutibu dalili na kupunguza makali, huku matibabu yanagusa dawa kama za malaria, pia za kuzuia maumivu.

**MGONJWA AJIELEZA**

Wiki hii, Nipashe ilizungumza na mgonjwa mmojawapo, akisimulia dalili kama anazopitia, ili ikiwasibu wengine watafute msaada wa matibabu mapema.

Stella Leonard (60), mkazi wa jijini Dar es Salaam, anaelezea hatua zake, jinsi ugonjwa ulivyomuanzia hadi alikofika sasa. Je, ni yepi amepitia na changamoto gani alizokumbana nazo katika kujiuguza hadi sasa?

Mama huyo anasimulia: "Tangu nikiwa mdogo umri wa miaka minane, nilikuwa kila siku naumwa mafindofindo kooni (tonsils), pia mafua ya kila siku na kupiga chafya mara kwa mara. Kwa hiyo, nimekuwa na hiyo historia ya aleji (uzio) hadi nikiwa na umri wa miaka 13, hali ilipokuwa mbaya zaidi.'

Anasema, alipoenda kutibiwa katika Hospitali ya KCMC iliyoko mjini Moshi, Kilimanjaro wakashauri afanyiwe operesheni kuyatoa hayo mafindofindo kooni, hatua iliyotekelezwa.

Stella anasimulia baada ya kupita kipindi ambacho hakumbuki sawasawa, kati ya mwaka mmoja na miwili, madaktari wakagundua tena vitu mithili ya nyama puani, navyo vikatolewa.


Anasema, baada ya hapo aliyojihisi kooni na puani ni kuna uwazi, hata akaanza kupata adha ya kila kitu akihisi kibaya, mfano vumbi linamuingia kirahisi.

"Nikawa nateseka sana kwa kuumwa, hivyo nikaandaliwa utaratibu kupelekwa Nairobi, Kenya kufanyiwa 'allegy Test', kipimo ambacho hapa nchini kilikuwa hakipo miaka hiyo ya 1980," anaeleza mama huyo, akitaja hatua hiyo ilimkuta katika umri wa usichana miaka 23.

Anakiri kutaabika sana na hilo, akiwa na ufafanuzi: "Wakati natolewa mafindofindo kooni, nilikuwa kwenye mafunzo Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makutopora na baadaye nikahamishiwa kambi ya JKT Oljoro. Wakati huo nikawa naumwa tu maafande hawanielewi, nyumbani hawanielewi, nikawa nachoka kila siku nina homa.

"Mwaka 1982 nikapelekwa hospitali moja jijini Nairobi inayoitwa MATA (MATA Miscondect Hospital). Nikafanyiwa hicho kipimo cha aleji na kunitajia vitu ambavyo

**Inaendelea Uk. 12**







# Anayeugua asimulia mazito yake, gharama na upekee usio kawaida

Inatoka Uk. 11

nikila ndio vinaniletea shida au nikikutana navyo kama vumbi, nikila mayai na baadhi ya dawa kama Penicilin na kadhalika ndio aleji inatokea."

Anasimulia, hospitalini hapo ikabidi wamuagizie dawa nchini Uingereza, anayoikumbuka iliwekwa kwenye chupa ya chai ,akawa anachomwa sindano zake na tatizo likapungua kidogo.

Stella anasimulia hatua iliyofuata katika miaka ya 1980, mateso mapya yakahamia mkononi ikimuathiri vidoleni na nyuma ya viganja kukiwapo vidonda, bila ya kumuambukiza mtu.

Anasema matibabui yake yakabidi kuhamishiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na baadaye hospitali ya Kilema mkoani Kilimanjaro, alikopatiwa dawa kutoka nchini Ujerumani, hata vidonda vikaweza kutulia.

**KASHESHE YA UJAUZITO**

Stella anaeleza mtihani mkubwa aliupata baada ya kubeba ujauzito mwaka 1996, akikukumbuka kuteseka sana ikiwamo kuvimba miguu mithili ya mwenye matendena akipoteza sura yake halisi

"Baadaye mtoto akawa siyo riziki. Lakini kilichokuwa kinawashangaza madaktari ni kwa nini nimevimba hivyo na mkojo una protini nyingi sana, lakini sijapata kifafa cha mimba, wala sina shinikizo la damu, yaani presha?.

"Baadaye nikapata mimba nyingine mwaka 1998, ikaonekana mtoto alikaukia tumboni, kwani alipofikia miezi mitatu, nilikuwa sisikii mapigo ya moyo.

"Ikafika miezi mitano hakuna kitu! 'Niliporudi kwa daktari wangu kunipima akasema anahisi mtoto amekufa. Madaktari wakasema inatokea lakini ni mara chache sana. Mtoto alipotolewa akawa amekaukia tumboni," anasimulia.

**DALILI ZENYE UTATA**

Mwaka 2011 anasema, akapata mtihani mwingine kimaisha, akiugua vitu tata, akijishangaa yu mweupe, ngozi yake nyeusi sana, uzito binafsi unampungua haraka sana. Hapo, akagundua maradhi hayo ya Lupus, yanadhuru meno binafsi.

Stella anaeleza atahari zake zaidi, kwamba yanadhuru mifupa ya nyonga na magoti, midomo inakauka, kuumwa viungo vyote mwilini, sura inabadilika kabisa.

"Nilipimwa sana hospitali ya Muhimbili, nikawa nahisi pengine nina ugonjwa wa UKIMWI. Watu wakawa wananiogopa. Aliyekuwa ananifahamu wala haniangalii mara mbili. Nikawa mvivu kazini, nikawa msahaulifu sana!.

"Kwenye mikutano nasinzia na kuonekana kitu cha ajabu! Lakini, nilikuwa nikijibidiisha kazini kufikia malengo. Nilikuwa mwili mkubwa, shepu nzuri lakini vyote hivyo vililiwa na ugonjwa huo," anasema.

**MWANA AMSAHAU MAMA**

Anasimulia mwaka 2013 ndipo familia yake ikaamua apelekwe nchini India kwa matibabu zaidi, ila kabla ya safari, binti huyo alirejea kutokea masomoni Malaysia na ndipo alipokutwa na madhila ya anayoyasimulia:

"Nikiwa Uwanja wa Ndege Dar (Uwanja Ndege Julius Nyerere) na baba yake kumpokea, alipowasili akamkimbilia baba yake akamkumbatia. Akamuuliza, 'mbona mama hakuja kunipokea? 'Baba yake akamjibu 'Si huyu hapa?'

"Binti akashangaa jinsi alivyomsahau mama yake, kwani alikuwa amedhoofu sana na kupoteza sura yake. Akalia sana nami nikalia pia."

Anaendeleza simulizi "Ule uzuri wangu umepotea hadi leo. Nilikuwa mweupe, mzuri. Nililia sana mtoto wangu kunisahau! Tulipotulia nyumbani nikamweleza, akanielewa. Baada ya kwenda India, Stella anasema akawataka madaktari wapime tena kama ana Ukimwi akiamini Tanzania wameshindwa kubaini, lakini madaktari hao kwa maelezo yake, walishahisi tatizo alilokuwa nalo.

'Majibu yaliporudi, madaktari wakaniuliza umesafirije wakati huna damu? Wakauliza nimekuja na mtu? Nikajibu mimi ni Mwafrika, nimeshaugua sana na kutumia fedha nyingi, nimekuja mwenyewe!,: anaeleza.

Mama huyo anafafanua ni wakati akawa anapata tatizo la upande mmoja wa uso wake nakuwa na ganzi, akaambiwa na matabibu kuwa linatokana na mshipa mmoja wa damu, unabana mshipa wa fahamu kichwani, nalo likiwa tatizo lingine.

"Nikiwa India nilikaa takriban siku 10 na kurudi Tanzania nikiwa nimebeba dawa nyingi pamoja na ripoti za daktari. Mwaka 2013, niliporipoti Muhimbili na kuwapatia ripoti ile, madaktari wakaniuliza nimejuaje kuwa nina Lupus? Nikawaambia nimejulia India, ndipo nikawapa ripoti zote," anasimulia.

Anasimulia tangu wakati huo akaendelea kupigana na Lupus akizingatia masharti ya vyakula, hasa kukwepa vyenye protini nyingi, kutopita juani na kumeza dawa nyingi zaidi ya vidonge sita kila siku, pasipo kukosa!

Kitaalamu, ugonjwa wa Lupus unatajwa unaweza kukoroga vitu vingi mwilini kwa mtu; ubongo, macho kuwa makavu, pia midomo, uti wa mgongo, vidole kubadilika rangi kuwa vyeusi.

Ngozi kukunjamana na kubadilika rangi, tumbo kujaa gesi, pia kizunguzungu, huku tafiti zikionyesha kwamba kila mtu anayo Lupus aina yake, ila dalili na namna ya kuumwa hutofautiana, mashambuliziyakigusa maeneo kama figo, mapafu, moyo na ubongo.

Stella anasema, binafsi anatafsiri ugonjwa Lupus 'ni kama shetani' anaporejea mateso na maumivu yake, akitaja nafuu anayoshukuru Lupus haijamuathiri viungo vya ndani ya mwili kama figo, moyo na mapafu.

Anafafanua wagonja wa Lupuz ndio hujitambua na kuelezwa namna ya kuhudumiwa.

**GHARAMA ZAKE TISHIO**

Gharama zake zikoje? Stella ana simulizi: "Kutibu Lupus ni gharama. Utauza kila ulicho nacho, ili ununue dawa na huduma zingine. Huwezi kula dawa bila kushiba sawasawa.' Anasema kurudi kwake nchini mwaka 2014 kutoka India, akaandamana na mzigo wa dawa na hadi sasa anaendelea kuagiza dawa kutoka India na Marekani, akiwatumia ndugu na marafiki wanaompenda.

"Kuishi na Lupus ni gharama, kwani watu wanaweza kukuchoka.... uwezo wote mlio nao, mtauza vitu ili mgonjwa aweze kuishi.

'Hata hivyo, nimegundua kuwa tatizo hili la Lupus siyo lipo Tanzania pekee bali hata majirani Kenya wanao wagonjwa. Na wagonjwa wa huko tunawasiliana nao na kupeana taarifa," anaeleza.

**MWANAFAMILIA MGONJWA**

Mama Stella anasema, katika familia yake yupo mgonjwa mmoja mtoto wa kike mwenye Lupus, mjukuu wa shangazi yake.

Ombi lake kwa serikali, ni kwamba ihusishe Lupus katika Bima ya Afya (NHIF) , kwani dawa na vipimo vyake vinawagharimu sana kila mwezi.



Ilivyo hali halisi ya madhara ya maradhi Lupus katika sehemu tofauti za mwili. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MAZINGIRA

# Jinsi wana- misitu Mwanza watetea hoja mbadala 'gesi haina pingamizi'

## • Watumiaji waorodhesha neema zilizopo

Na Anthony Gervas, Mwanza

KITAFA na kimataifa hadi sasa kuna hoja inayotamba katika kona nyingi kwamba jamii ipambane kutetea maliasili yake na katika namna ya pekee kulinda misitu.

Hilo daima halijawahi kuwa ajenda mpya tangu siku hiyo, hadi sasa inashamiri kila mahali, leo dunia inatekeleza Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 kuhusu mazingira. Nchini Tanzania, nako kuna historia ya hekaheka kupitia sura na hatua nyingi.

Kunakumbukwa zama fulani kuwepo operesheni 'kata mti panda miti' kwa maana ya kila mti unaokatwa, nafasi yake izibwe kwa kupandwa zaidi ya mti mmoja.

Ni hatua yenye ushuhuda halisi wakati fulani zaidi ya miongo miwili kupita wilayani Rungwe hasa katika tarafa ya Busokelo, zama hizo kulivyoonyeshwa mwamko ngazi ya juu wa wakazi wake katika 'kata mti panda mti,'

Mahali hapo sasa jiografia yake imeenguliwa kutoka jimbo la uchaguzi Rungwe, ikiwa jimbo Busokelo na baadaye kupewa hadhi zaidi, Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe.

Katika muundo wa kiserikali, tangu zama za mwaka 1995 suala la mazingira limepandishwa hadhi na kuwekwa kwenye ngazi ya wizara tena likiwa chini ya usimamizi wa mamlaka ya juu kitaifa.

Ni baada ya hapo kukashuhudiwa kuundwa nyenzo nyingi za kusimamia mazingira, hali inayoendana na kuudwa wakala wa kitaifa, ikiwemo Wakala wa Huduma za Misitu (DFS).

Pia, Rais Benjamin Mkapa, wakati fulani katika zama za uongozi wake, aliwaagiza wakuu wa wilaya kusimamia kuzalisha miti kwa wingi, kwamba ingekuwa kigezo chake kutathmini ufanisi wa utumishi wao.



Mkaa ukiwa tayari kuuzwa. **PICHA: MAKTABA.**

### KINACHOENDELEA MWANZA

Ofisa Mhifadhi wa Wakala wa Misitu wilayani Nyamagana jijini Mwanza, Justice Mmari, anabainisha kuwa uzalishaji nishati mbadala ya gesi umepunguza utumiaji wa mkaa na ukataji wa miti ovyo wilayani humo.

Mmari anasema, wananchi wenye vipato vya chini bado wanaona matumizi ya nishati gesi ni makubwa kuliko ya mkaa, kutokana na bei za kununua na kujaza ziko juu.

Anaeleza mazingira linganishi kwamba bei kuanzia debe moja inauzwa kati ya Sh. 5,000 hadi Sh. 8,000 kulingana na maeneo husika na mkaa unaopatikana haukidhi matumizi ya muda mrefu.

Ofisa huyo anasema uharibifu wa mazingira, pia unachangiwa na wananchi kukata miti holela na kufyeka misitu kwa ajili ya kuchoma mkaa, hivyo serikali inalazimika kufanya jitihada za kupambana na changamoto hiyo.

Anafafanua kwamba, kuwepo gesi kungewasaidia kupunguza heka heka za operesheni kuwasaka na kuwakamata wahalifu wa ukataji miti kutengeneza mkaa kwenye hifadhi za DFS.

### MAGEUZI YA TABIANCHI

Ofisa huyo anasema, ukataji holela wa miti na misitu, unachangia kuwepo madhara ya mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo mvua kuchelewa kunyesha na kwa kiwango kisichoridhisha, kukiwapo mmomonyoko wa udongo.

Anasema katika sekta yao wilayani Nyamagana, wameanzisha bustani za uoteshaji miti na kuwagawia bure wananchi, pia taasisi mbalimbali binafsi na kiserikali kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao.

Taasisi zinazopata miche hiyo ya bure kuu ni za umma zikiwamo shule za msingi na sekondari, makanisa na kutoa elimu ya upandaji miti, hali kadhalika utunzaji mazingira.

Mmari anajisifu kwamba wameshanufaika nazo kimazingira, akizitaja ni pamoja na kwenye mustakabali wa uchumi kama vile kuvuna mbao, kupata hewa safi na, pia kuendelea kuwa na uoto wa asili.

### ILIVYO SAFARI MBADALA

Hadi sasa kunasifiwa kuwapo mbadala wa kuni, kwa kutumia gesi ambayo imefika sehemu nyingi na hasa mijini, sifa yake mojawapo ni kuwapo gharama ndogo ya matumizi, kupika haraka kuliko na lile linaloigusa Wakala wa Misitu, kulinda mazingira yabaki salama.

Ni huduma inayoonyesha ufanisi penye biashara, hadi mghahawa na hoteli ambako sasa imechukua nafasi kubwa wakiungana katika falsafa hiyo. Mamalishe, Fatma Seif, mkazi wa jijini Mwanza anatoa ushuhuda wa manufaa .

Fatma anaitaja nishati hiyo mbadala, kwamba wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutambua vyema matumizi hayo. Anaendelea kufafanua:"Ina matumizi ya chini zaidi ya mkaa, ila wananchi hawana uelewa zaidi juu ya kutambua matumizi yake. Mfano, unapika ugali kwa dakika tano tu, tofauti na mkaa unatumia dakika 15 hadi 20 kuivisha."

Pia, anadokeza kuwa nyama inaivishwa dakika 30, huku mkaa unatumia saa moja, hivyo imewapa nafuu kinamama wengi kuanzia ngazi ya familia wanajikita kwenye gesi.

Vilevile, nishati imebadilisha maisha ya familia nyingi, kutokana na kuokoa muda wa kupika chakula, ili watu waweze kuendelea na shughuli zingine za uzalishaji mali.

Anafafanua kuwa biashara ya kisasa daima inaenda sambamba na teknolojia ya gesi ikiwapa faida, inachafua mikono kama ilivyo kwa mtumiaji mkaa, ikiendana na joto kidogo, inanusuru mazingira, mavazi, mikono na kuondoa haraka mazingira yasiyo rafiki kwa mpikaji na mteja.

Mama huyo anasema mkaa una gharama kubwa ya matumizi, ila wananchi wengi hawapigi hesabu sahihi ya uwiano ulioko. Kuhusu bajeti yake, akieleza mtungi mkubwa unaonunuliwa Sh. 180,000, anaujaza na unaisha kwa Sh.100, 000 na anautumia mwezi mzima kwenye mghahawa wake.

Hivyo, anachanganua kwamba gharama za mkaa bado ni kubwa hasa kwa wanaonunua rejareja, mathalan kwenye kopo la Sh. 1000.

Anasema yeye hupika pia chapati, maandazi na vitafunwa vingine kwa gesi, mkaa kwake ni huduma ya dharura penye ulazima.

Rai yake ni kwamba, serikali bado ina jukumu la kuelimisha zaidi jamii matumizi ya nishati hiyo, ili wanajamii wabadilike, wakiwemo wananchi vijijini ambako matumzi ya kuni yameshamiri.

Anafafanua baadhi ya athari zilizoko ni kwamba mkaa unaumiza kifua cha mtumiaji na wanaozingira, kutokana na vumbi na joto linaloathiri mandhari tajwa, hivyo gesi inabaki salama kwa afya ya binadamu.



Jiko la gesi likitumika kupika. **PICHA; MTANDAO.**

AFYA

# Maisha mapya Hospitali ya Rufani Mwananyamala sasa iki'ngara upya

## •Orodha ndefu ya madakatri bingwa



Rais Samia, alipotembelea Hospitali ya Rufani Mwananyamala, jijini Dar es Salaam.

**Na Halfani Chusi**

JIJI la Dar es Salaam, lenye wilaya tano, kwa sasa lina hospitali kuu tatu za rufani ngazi ya mikoa; Temeke, Amana na Mwananyamala, zikitokea historia ya kuwa zahanati, wastani wa miongo mitano iliyopita.

Katika orodha hiyo ikiwamo ya Mnazi Mmoja, ambako nako sasa ni hospitali kuifanya jiji la Dar es Salama kuwa na hospitali nyingi za kiserikali, kama ilivyo kwa nyinginezo, Kitunda na Sinza.

Vivyo hivyo, daima mtu anaposikia hospitali fulani ina mafanikio lukuki, daima picha inayokuja kichwani ni ya furaha na amani, moyo unafarijika zaidi kumuona mwenye shida ya kiafya anatibiwa bila ya shaka.

Hapo ndipo inapotajwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala iliyoko wilayani Kinondoni, ikiwa katika sura ya ufanisi, wahusika wake wanaangukia katika hulka ya tabasamu.

Hadhi yake ya sasa, Nipashe imeshuhudia ikiendana na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi kirefu katika hospitali, kumaliza vikwazo kadhaa ambavyo vilikuwa vinaikabili hospitali hiyo.

Katibu wa Afya Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwananyamala, Rajabu Kaseke, anafafanua kuwa awali Hospitali ya Mwanayamla, ilikabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa katika fani mbalimbali, vyumba vya uzazi, wajawazito na watoto.

"Kwa sasa, hayo yote yamepatiwa ufumbuzi na hayo anathibitisha Katibu Kaseke," anatamka na kuongeza :"Hospitali yetu ya Mwananyamala kwa sasa ni kubwa na ina madaktari bingwa 19 wa fani tofauti."

"Tumefanikiwa kuwa na jengo kubwa la ghorofa kwa ajili ya kinamama wajawazito na watoto, kitu ambacho mwanzoni tulikuwa hatuna. Kwa hiyo, wagonjwa walikuwa wanapata shida, wengine tulikuwa tunalazimika kuwapeleka hospitali ya Muhimbili, kwa ajili ya udogo wa eneo katika hospitali yetu," anaeleza.

Pia, anasema kwa sasa Hospitali ya Rufani Mwananyamala, inatoa huduma za kisasa zaidi wakiwapo madaktari bingwa wa pua, koo, ngozi, mifupa, madaktari bingwa, kinamama na watoto, pamoja na magonjwa ambayo awali hayakupatiwi ufumbuzi mahali hapo.

"Hospitali ya Mwananyamala ya leo, sio sawa na hospitali ya miaka kadhaa nyuma. Kwa sasa, hospitali hii imekuwa hospitali ya mkoa na ina madaktari bingwa 19, wa fani tofauti.

"Pia, kwa sasa tumefanikiwa kuwa na jengo kubwa la ghorofa kwa ajili ya kinamama wajawazito na watoto kitu ambacho mwanzoni tulikuwa hatuna, kwa hiyo wagonjwa walikuwa wanapata shida, hivyo wengine tulikuwa tunalazimika kuwapeleka hospitali ya Muhimbili," anasema.

**UJUMBE MAALUM**

Katibu wa Afya, anaendeleza rai kwa watu kujenga utamaduni wa kukata bima, ili iwe rahisi kwao kumudu gharama za matibabu, pindi wanapopatwa na matatizo.

"Niwaombe watu wawe na utaratibu wa kukata bima, ili iwe rahisi mtu anapopata tatizo kuhudumiwa bila ya shaka yoyote, utakuta mtu anaumwa hawezi kumudu gharama za matibabu.

"Hivyo, inalazimika hospitali iingilie jukumu la kumsaidia na akishapona hakumbuki tena kulipa, kwa hiyo niwaombe watu wajenge utaratibu wakukata bima, ili kujiweka katika mazingira ya kutibiwa, bila ya shida yoyote," anasema.

Rajabu anasisitiza umuhimu wa jamii kuwa na huduma za bima ya afya, ili kutoa fursa ya kutibiwa wakati wowote pindi anapopatawa na shida ya matiabu, iwe hospitalini Mwananyamala, au eneo lingine la mbali.

**SHIDA INAYOTAWALA SASA**

Katibu Rajabu, anasema pia wana changamoto za kutekeleza majukumu yao hospitalini, ikiwamo wanaofikishwa mahali hapo hawajitambui, hali inayowafanya washindwe kujua namna ya kumuunganisha na ndugu, pia jamaa zake.

Aidha, kuna baadhi ya wagonjwa wanaotibiwa hospitalini humo, wanashindwa kulipa madeni hata baada ya kutibiwa na kupona, ilhali wameshatibiwa na mpaka sasa ndugu zao hawajapatikana.

Rajabu anaeleza kwamba watu hao bado wanaendelea kutumia gharama za hospitali, wakibakiwa na changamoto, kwa kuwa ni ngumu kumfukuza kutoka wodini.

"Unakuta mgonjwa amefikishwa hapa yupo hoi hoi na jeshi la polisi, aidha alipata ajali au amepigwa na vibaka hajitambui amepoteza kumbukumbu, hakumbuki hata namba ya simu ya ndugu zake.

"Wagonjwa wa namna hii wanatupa changamoto sana, inabidi hospitali iingie gharama ya kumhudumia mgonjwa, mpaka apate nafuu ajitambue ili awatambulishe ndugu zake na ikitokea amekufa, basi ndio hasara ya hospitali kwa sababu inabidi itumie gharama kwenda kumzika," anafafanua.

Anaeleza maofisa wa ustawi wa jamii, wapo hospitalini kuwasaidia wagonjwa wasio na ndugu na anabainisha wamekuwa wakiwasaidia pale wanapokutana na chagamoto hizo wanawasaidia kifedha, pamoja na chakula kwa wagonjwa hao.

Pia, anataja wamekuwa wakitusaidia kuwafikisha nyumbani wagonjwa waliofikishwa mahali hapo, wakiwa hawajitambui na baadae wakatibiwa na kupata nafuu, hata wakasaidia kuwapeleka hadi makwao.

**MAONI YA WAKAZI JIRANI**

Mkazi wa Mwananyamala, ambaye pia anapata matibabu katika hospitali hiyo, Jumanne Mbayugwa, anakiri kuwapo nafuu ya matibabu hospitali hapo, akitofautisha na ilivyokuwa awali.

"Zamani ulikuwa ukija hapa ukiwa una mtoto anaumwa, unaweza ukakosa pa kumlaza au ukapewa kibali kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili na gharama ikaongezeka," anaeleza.

Jumane anafafanua kuwa, zamani wagonjwa wengi walilazimika kupelekwa Hospitali ya Muhimbili, sasa ni tatizo lililotoweka.

Vilevile, mkazi mwingine, Jackob Raymond, anaeleza kufurahia uwepo wa madaktari bingwa wa ngozi, anabainisha kuwalazimu kusafiri hadi hospitalini, hata iliwagharimu.



Sehemu ya Hospitali ya Rufani Mwananyamala, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





# DIT yatangaza ubunifu wa wanafunzi wake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Teknolojia Dar es Saalam (DIT), kupitia kampuni yake tanzu imeanza kutangaza bunifu zake zinazofanywa na wanafunzi wake ili kwenda kujibu changamoto zilizoko katika jamii.

Meneja Masoko wa Kampuni ya DIT, Agnes Kimwaga, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, wakati wa maonyesho ya ubunifu mbalimbali uliofanywa na taasisi hiyo yaliyofanyika kwenye viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Alisema, Taasisi ya Teknolojia Dar es Saalam imeanzisha kampuni hiyo ambayo itawezesha kuuzwa kwa bunifu mbalimbali ambazo zimekuwa zinafanywa na wanafunzi wake.

"Kampuni hii itauza bunifu zote ambazo zimefanywa kwa kuzipeleka sokoni na kuziuza badala ya kubaki katika makabati bila kuwa na tija," alisema Kimwaga.

Alisema kabla ya kuanzishwa kampuni hiyo tanzu bunifu nyingi zilikuwa zinabaki na kufungiwa kwenye makabati ofisini bili kuwa na manufaa kwa taasisi na jamii.

"Tumekuwa tukiandaa bunifu mbalimbali kupitia wanafunzi wetu, lakini zinaishia kwenye makabati sasa tumeamua kuzifanya ziwe biashara bunifu zote ili kwenda kujibu changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii," alisisitiza Kiwanga.

Kadhalika, alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya bunifu nyingi ambazo zinajibu changamoto mbalimbali katika jamii kwenye sekta mbalimbali ikiwamo miundombinu.

"Tumekuwa tukifanya bunifu za taa kwenye vivuko vya barabara ambazo tunaweza kufanya biashara na Wakala wa Barabara Nchini (TANROAD) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), badala ya kubaki nazo.

"Lakini hivi sasa tumebuni mfumo wa kufuatilia miradi mbalimbali, tumebuni kifaa cha kubebea watoto njiti ambacho kinaweza kutumia hata katika zahanati ngazi ya kijiji kwa gharama nafuu, lakini pia kuna kifaa cha kusafisha maji ambacho kwa maeneo ya vijijini kinafaa kwani ukitumia unaweza kuyanywa maji bila kuchemsha," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, aliitaka taasisi hiyo kusajili bunifu zake ili kuzilinda dhidi ya watu wenye tabia ya kuiba bunifu hizo.

Mtaka, alisema kumekuwapo na watu ambao wamekuwa wazuri kuiba bunifu za watu wengine, kama taasisi hiyo haitakuwa makini inaweza kujikuta katika wakati mgumu.

"Ni wapongeze kwa bunifu mnazofanya, lakini mnapaswa kuzisajili na kuanza kuzifanyia kazi au kuziuza kwani hizo bunifu ni fedha hamna sababu ya kuendelea kulalamika wakati mmekaa na bunifu kama hizi kwenye makabati," alisema.

Vilevile, aliwataka wakuu wa wilaya za Dodoma kutumia taasisi hiyo ili kupata mifumo mbalimbali itakayo wasaidia kujibu kero mbalimbali katika maeneo yao.

"Nawakaribisheni DIT katika Mkoa wa Dodoma na mimi naomba tuanze kuutumia mfumo wenu huu mliobuni wa kusajili bodaboda kwani hapa kwetu tunao takribani 10,000," alisema Mtaka.



Msemaji Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Baraza hilo, Sheikh Khamis Mataka, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, alipotoa pongezi kwa serikali kutokana na bajeti ya mwaka 2022/2023 kuwagusa wananchi wa hali za chini. **PICHA PETER MKWAVILA**

## Msako kuondoa gereji bubu, malori katikati Jiji warindima

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeanza kufanya msako usiku na mchana kwa ajili ya kuondoa gereji bubu na malori yanayoegeshwa katikati ya mji ili kuliweka Jiji katika mazingira safi.

Msako huo ni pamoja na kuwatoza faini Sh. 50,000 hadi 300,000 kwa wale watakaobainika kuwa na gereji bubu na malori yanayopaki kinyume cha sheria.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi.

Alisema Halmashauri ya Jiji imelazimika kufanya doria hiyo kutokana na kubainika kuwapo kwa gereji na malori katikati ya mji ambayo hayatakiwi kuwapo.

Alisema tayari halmashauri ya jiji imeshatenga maeneo rasmi kwa ajili ya gereji pamoja na eneo la kuegesha malori eneo la Nanenane na Nala.

Kimaro alisema doria hiyo itakuwa ya kudumu na itawashirikisha wakuu wote wa idara wa halmashauri ya jiji kwa kushirikiana na kamati za mazingira za mitaa na kata na maofisa afya.

Pia, aliwataka wafanyabiashara wenye maduka kuhakikisha maeneo yao yanakuwa katika mazingira yaliyo safi kwa muda wote badala ya kusubiri kutozwa faini.

"Jiji halitasita kuwakamata wale wote watakaokiuka sheria na utaratibu wa mazingira tutahakikisha tunafanya msako kwa muda wote lengo kuliweka jiji hili katika mazingira safi," alisema.

Kadhalika, aliwakumbusha wakazi wote waliopo kando kando na barabara za jiji kuwa mabalozi wa kutunza na kuilinda miundombinu iliyoko.

**Alisema tayari halmashauri ya jiji imeshatenga maeneo rasmi kwa ajili ya gereji pamoja na eneo la kuegesha malori eneo la Nanenane na Nala.**

# UDOM yabuni mfumo kuzuia ajali barabarani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM), Idara ya Ubunifu na Ujasiriamali kimebuni mfumo wa kuzuia ajali katika makutano ya vivuko vya reli na barabara ujulikanao kama 'Direction Railway Automatic System' ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na ajali.

Hayo yalisemwa na Mhadhiri wa chuo hicho, Hamad Mtani, katika maonyesho ya Elimu ya Vyuo vya Ufundi yanayofanyika katika Uwanja wa Jamhuri.

Mtani, alisema kitengo hicho waliamua kubuni mfumo huo baada ya kufanya utafiti na kugundua maeneo ya vivuko vya reli na barabara kumekuwa na ajali nyingi zinazotokea na kusababisha vifo.

"Tumebuni mfumo huu ili kuhakikisha ajali za kwenye vivuko zinapungua au kumalizika kabisa kwa sababu mfumo huu utakuwa unajifunga mara treni inapokaribia eneo la kivuko," alisema Mtani.

Akielezea namna mfumo huo unavyofanya kazi, Mtani alisema utakuwa na geti ambalo litakuwa likifunga treni inapokaribia kwenye kivuko hata kama mtu hatakuwapo eneo hilo.

Alisema kikawaida katika mazingira ambayo kuna makutano ya reli mara nyingi zimekuwa zikitokea ajali kutokana na watu wanaoendesha magari wanakuwa wakijisahau ikiwamo kwenda mwendo kasi wanapofika katika eneo hilo.

Alisema mfumo huo utakuwa unawaonyesha watu wakiwa mbali kupitia taa ambayo itawaka kuashiria kuwa kuna treni inakuja na dereva anapaswa kusimama.

"Mfumo huo unafanya kazi ya kufunga geti unasensi ambazo wakati treni inakaribia kwenye makutano kunakuwa na taa zinazoashiria gari isimame ili kupisha treni ipite," alisema.

Alisema mfumo huo pia nyakati za usiku unaweza kufanya kazi bila ya uwapo wa mtu kutokana na kufanya kazi kwa kujiendesha bila ulazima wa kuwapo mtu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Ubunifu na Ujasiriamali wa Chuo Kikuu Dodoma, Dk. Alex Mongi, alisema mfumo huo ni muhimu kuwapo kwenye vivuko hivyo kwa kuwa utasaidia kupunguza ajali pamoja na kuwakumbusha watu kuwa makini wanapofika eneo la kivuko.

Dk. Mongi alisema bunifu hizo ambazo zimefanywa na walimu, wanafunzi zipo katika hatua mbalimbali ili ziweze kuboreshwa na kuhamia hatua nyingine ambayo itaanza kutumika katika maeneo mbalimbali.

Alisema lengo la kubuni mifumo hiyo ni pamoja na kutaka kupunguza changamoto ambazo zinajitokeza katika maeneo mbalimbali na kuisaidia jamii.

Kadhalika, alisema anaishukuru serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), kusaidia kuendeleza bunifu mbalimbali za wanafunzi.





# CHADEMA: Wanaobeza maridhiano wapuuzwe

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Nyasa, umewataka wanachama wa chama hicho na Watanzania kuwapuuza watu wanaobeza maridhiano yanayofanywa na viongozi wakuu wa chama hicho na serikali.

Hivi karibuni viongozi wa chama hicho wakiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe, walikutana na kufanya mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na baadhi ya viongozi wa CCM Taifa kwa lengo kufanya maridhiano.

"Baada ya viongozi hao kukutana, baadhi ya wananchi walianza kuwabeza viongozi hao wakidai kuwa 'wamelambishwa asali' na serikali na maneno mengi yaliibuka hasa kwenye mitandao ya kijamii."

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Gwamaka Mbugi, aliyasema hayo juzi alipozungumza kwenye Mkutano Mkuu wa dharura wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya uliokuwa na lengo la kufanya uchaguzi wa kuziba nafasi za viongozi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema maridhiano yanayofanywa na viongozi sio jambo baya kwa maelezo kuwa hawajaanza kutafuta maridhiano hayo kwenye utawala wa Rais Samia bali tangu kipindi cha Utawala wa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema awali walikuwa wanashindwa kufikia hatua hiyo kutokana na aina ya utawala uliokuwapo ambao ulikuwa unawafanyia mambo yasiyokuwa ya kawaida ikiwamo kuwekwa ndani na kuzuia mikutano ya kikatiba.

Alisema kama kukutana na watesi ni kulambishwa asali basi mtu wa kwanza kulambishwa alikuwa Rais wa awamu ya kwanza wa Tanzania, hayati Julius Nyerere ambaye mwaka 1954 mpaka 1958 alienda Umoja wa Mataifa (UN) kudai Uhuru wa Tanganyika kwa wakoloni ambao walikuwa watesi wake.

Alisema pia, Rais wa kwanza wa Jumhuri ya Afrika Kusini, Nelson Mandela, alifungwa na makaburu miaka 27, lakini alipotoka watu wa kwanza kukutana nao kufanya maridhiano walikuwa ni watesi wake hao.

"Mbowe kukutana na serikali sio tatizo hata kidogo, naomba tuyapuuze maneno ya mtaani na badala yake tuunge mkono maridhiano yana nia njema kwa Watanzania wote na nawaomba tuendelee kuunga mkono harakati za viongozi wetu," alisema Mbugi.

Akizungumzia suala Katiba Mpya, Mbughi aliwataka viongozi wa CHADEMA kusoma na kujua upungufu wa Katiba iliyopo na kuwaeleza wananchi ili harakati za kudai mabadiliko ziongezeke nchini.

Naye Katibu wa Baraza la Vijana wa chama hicho (BAVICHA), Mkoa wa Mbeya, Emily Mwakilembe, aliwataka wafuasi wa chama hicho kujenga utamaduni wa kuheshimu viongozi wa juu akisisitiza kuwa hakuna mtu aliyewahi kufanikiwa kwa kutukana viongozi.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wafuasi wa chama hicho kutolinda heshima ya viongozi hali ambayo inaharibu taswira ya chama chao.

Mwenyekiti Baraza la Wanawake la chama hicho mkoa wa Mbeya (BAWACHA), Elizabeth Mwakimomo, alisikitishwa na idadi ndogo ya wanawake katika Wilaya Chunya huku akiwataka wanawake kufanya kazi ya kuendeleza chama hicho.

Alisema uhai na ushindi wa chama hicho katika chaguzi mbalimbali unategemea wanawake na wasitarajie ushindi katika nafasi mbalimbali kuwa na wanawake.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akitoa maelekezo kwa wataalamu wa kilimo kuhusu umuhimu wa uzalishaji wa kitaalamu wa zao la mahindi, wakati wa kilele cha maonyesho ya kilimo biashara, kwenye mashamba ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# BRELA yaita wakurugenzi kuwasilisha taarifa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka Wakurugenzi na wamiliki wa kampuni nchini, kuendelea kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa kwa wakati ili kuwa na uwazi na uwajibikaji.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa sehemu ya kampuni wa BRELA, Leticia Zavu, wakati wa warsha maalum ya uhamasishaji wadau kuhusu kanuni za wamiliki manufaa, inayofanyika iliyofanyika kwa siku mbili jijini Mbeya.

Zavu alisema kuwa ushiriki wa wadau katika warsha hiyo umetoa mwanga katika kuelekea mapinduzi ya uwekezaji nchini, huku akisisitiza uwajibikaji unaenda sambamba na uwazi katika utekelezaji wa majukumu, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

"Wadau mnapaswa kutoa elimu hii kwa jamii inayowazunguka, kwa sababu taarifa zinalenga kumfahamu mmiliki halisi na chanzo cha fedha za kampuni husika, kwa usalama wa nchi na kupunguza mianya ya ubadhilifu miongoni mwa kampuni, hivyo mkawe chachu katika kufanikisha uwasilishaji wa taarifa hizi ndani ya muda uliopangwa," alisema Zavu.

Hata hivyo, Zavu alifafanua kuwa taarifa hizo ni za siri na kwamba wanaendelea kuzichakata na wanaendelea kufanya kazi kwa umakini.

Aliongeza kuwa mmiliki Manufaa anayepaswa kuwasilisha taarifa zake BRELA ni anayemiliki kuanzia asilimia tano na zaidi ya uwekezaji kwenye kampuni au kushiriki kufanya maamuzi kwenye kampuni moja kwa moja na taarifa zao zinatakiwa kuwasilishwa kupitia mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Manufaa unaopatikana kwenye tovuti ya BRELA.

Kwa upande wake Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema ofisi yake ipo tayari kuhudumia kampuni zote zitakazofika kwa ajili ya kusajili biashara zao au kubadilisha umiliki wa hisa.

# Ekari 100,000 zatengwa Chunya kilimo cha soya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imetenga eneo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 100,000 katika Wilaya ya Chunya kwa ajili ya kilimo cha zao la soya.

Uamuzi huo umetokana na serikali kupata soko la uhakika katika nchi za Bara la Asia ikiwamo China ambako inahitajika kwa wingi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitangaza hatua hiyo ya serikali wakati akizungumza kwenye kilele cha Maonyesho ya Kilimo Biashara ambayo yaliandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole.

Homera alisema, baada ya kupatikana kwa eneo hilo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, wanatarajiwa kuwasili mkoani humo kwa ajili ya kuliona na kuanza uwekaji wa miundombinu inayohitajika kwa kilimo hicho.

"Tayari serikali imeandaa eneo kubwa lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 100,000 ambazo zipo wilayani Chunya, eneo hili ni mahususi kwa kilimo cha soya na mazao mengine ambayo tumepata soko la uhakika barani Asia," alisisitiza Homera.

Aliwataka wananchi kuanza kujiandikisha ili wakapewe sehemu ya eneo hilo kwa ajili ya kuanza kilimo hicho na kuwa wa hiyo ni fursa kubwa kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya.

Akizungumzia uendelezaji wa eneo hilo, Homera alisema tayari serikali imeandaa fedha na vifaa kwa ajili ya kusafisha eneo tayari kwa kilimo.

Vile vile, wamepatikana wataalam kutoka nchini China watakaosaidiana na serikali kuhakikisha kilimo hicho kinakuwa na tija.

"Wananchi mnachotakiwa kufanya ni kujiandikisha tu ili mpewe mashamba mkalime, lakini maandalizi mengine yote serikali yenu ya awamu ya sita itashughulikia," alisema Homera.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo, Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, alieleza namna ambavyo Mkoa wa Mbeya umejizatiti kutoa huduma bora ya ughani kwa wananchi.

Alisema serikali imeshatoa vifaa vya usafiri wa pikipiki kwa maofisa ugani wote wa kata ili waweze kuwafikia wakulima na kuwaelimisha kuhusu mbinu za kilimo bora.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kituo chake kimeshafanya utafiti wa mbegu bora za mazao mbalimbali ikiwamo soya ambazo zikitumiwa na wakulima wanao uwezo wa kupata mazao mengi na yenye tija.

Alisema kuwa utafiti wa kina uliofanyika umefanikisha kupatikana kwa mbegu bora zinazohimili maradhi, ukame na kutoa mazao mengi na wananchi watakaotumia mbegu kutoka TARI watarajie kuzalisha kwa tija. Baadhi ya wananchi waliofika kwenye maonyesho ya kilimo biashara, walisema maonyesho hayo yamewasaidia kutambua mbinu za kilimo bora na zinazofaa kupandwa kwenye mashamba yao katika kipindi hiki cha mabadiliko ya tabianchi.

Miongoni mwa wananchi hao ni Elizabeth Mbeyanje ambaye alisema amejifunza mbinu mbalimbali ikiwamo kutambua mbolea inayofaa kwa kilimo cha mahindi kwenye shamba lake na namna ya kupanda mbegu bora ili apate mazao mengi.



# Waziri aona fursa uchakataji wa asali

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uwezeshaji kiuchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema ujenzi wa vituo vya kuchakata mazao yanayotokana na asali kwa kiasi kikubwa utawawezesha wajasiriamali kuingia katika masoko ya kimataifa.

Aliyasema hayo jana alipotembelea kituo cha kusarifu na kuchakata mazao yanayotokana na asali huko Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Waziri Soraga alisema serikali imekubali kutenga zaidi ya Sh. milioni 960 kwa ajili ya wazalishaji wa mazao ya asali ili kuingia katika soko la kimataifa.

"Zanzibar kuna wazalishaji wengi wa asali ambao wamepatiwa mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za uzalishaji wa asali pamoja na ufugaji wa nyuki ili kutoa mazao mengi ya asali.

"Nimefurahishwa na kasi ya ujenzi wa kituo cha kusarifu na kuchakata mazao yanayotokana na asali ambapo serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya wafugaji kuingia katika mbinu za kisasa za kufuga nyuki ili kuzalisha asali itakayoingia
katika soko la kimataifa," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab, aliwataka wajasiriamali na wazalishaji wa asali kujipanga na kuchangamkia fedha ambazo zimetengwa kwa kazi hiyo.

"Kwa mara ya kwanza, serikali imetenga fedha kwa wajasiriamali wafugaji na wazalishaji wa asali kwa lengo la kuona wanatekeleza majukumu yao kwa kutumia mbinu za kisasa zitakazowaingiza katika soko la kimataifa," alisema.

Jumla ya vituo viwili vya kusarifu na kuchakata asali vinatarajiwa kujengwa nchini huko Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja pamoja na Pujini Pemba.

# CHADEMA walaani Shamte kudaiwa kuteswa, kujeruhiwa

Na Mwandishi Wetu,
ZANZIBAR

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimelaani kitendo alichofanyiwa mwanasiasa mkongwe, Baraka Shamte, aliyedaiwa cha kutekwa na watu wasiojulikana, kumtesa na kumjeruhi kisha kumtupa eneo la Unguja Ukuu Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Salum Mwalimu, alisema CHADEMA haiwezi kuvumilia wala kufumbia macho vitendo vya aina hiyo.

Alisema vitendo hivyo siyo tu vinahatarisha usalama wa raia na uhuru wao, bali ni kinyume cha ungwana na ustaarabu wa maisha ya Mzanzibar.

"Uchunguzi wa Jeshi la Polisi ambao liliahidi kuufanya, uwe wa haraka na kutoa taarifa kwa umma nini kilitokea, wahusika lengo lao lilikuwa ni nini?" alisema.

Mwalimu alisema ameona tamko la serikali la kulaani kitendo hicho na wameahidi kulichunguza.

"Hadi anakutwa na kadhia hiyo, Baraka Shamte alikuwa ni kada maarufu na mkongwe wa CCM, hivi karibuni ameonekana katika mitandao ya kijamii akikosoa mwenendo wa Serikali ya CCM na sera zake za uwekezaji, CHADEMA inayapitia na kuchambua maudhui ya maoni hayo na itayatolea msimamo wake kwa umma," alisema.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Abdalla Hussein Mussa, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi dhidi ya tukio hilo.

Kamanda Hussein alisema kuwa Jumamosi Shamte aliitwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano kutokana na kutoa kauli za uchochezi dhidi ya matamshi ya viongozi wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa njia ya mtandao.

Alisema Shamte alihojiwa na kuachiliwa kwa dhamana kwa ajili ya kupisha uchunguzi zaidi wa tuhuma zinazomkabili na Juni 12 mwaka huu, majira ya saa 12 walipokea taarifa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhusu kujeruhiwa kwake baada ya kupigwa na watu wasiojulikana.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, Jeshi la Polisi lilifika hospitalini huko kwa mahojiano zaidi na majeruhi alieleza kuwa alitekwa na watu sita asiowafahamu nyumbani kwake Mkunazini mjini Unguja na kumtelekeza Unguja Ukuu baada ya kumjeruhi.

"Jeshi la Polisi linafuatilia zaidi kuhusiana na tukio hili na uchunguzi wa taarifa hizo ukikamilika zitatolewa kwa vyombo vya habari," alisema.

Mwishoni mwa wik iliyopita, Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Kamati Maalum CCM Zanzibar, Caterine Peter Nao, alikanusha vikali matamshi yaliyotolewa na kada huyo na kueleza kuwa yanakwenda kinyume cha maadili ya wanachama.

Baraka Shamte ni mtoto wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa serikali ya kikoloni kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba, ambaye ni Balozi wa Kodi, Zulfa Omar Mmaka (wapili kulia), akiwa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wakitoa elimu ya kuhakiki stempu kwenye kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafafanua majukumu ya Tume ya Pamoja Usimamizi Fedha

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

SERIKALI imesema Tume ya Pamoja ya Usimamizi wa Fedha ipo kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano na miongoni mwa majukumu yake ni kuweka usimamizi mzuri wa mgawanyo wa matumizi ya rasilimali na fedha zinazotokana na mikopo ya nje.

Akitoa ufafanuzi kuhusu mapendekezo ya bajeti ya serikali iliyowasilishwa juzi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema makao makuu ya tume hiyo yapo Zanzibar lakini wananchi wengi hawafahamu majukumu yake kwa sababu haijaanza kutekeleza majukumu yake vizuri.

Alisema Serikali ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wajumbe watakaounda tume hiyo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano.

Alisema nafasi ya Mtendaji Mkuu wa tume kutoka Zanzibar ipo wazi baada ya Mtendaji Mkuu kufariki dunia kwa ajali miezi mitatu iliyopita.

"Serikali ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za kuteua majina ya wajumbe wanaounda tume hii watakaoungana na upande wa Jamhuri ya Muungano ili kutekeleza majukumu yake," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya LEMBENI**
**Kituo cha LEMBENI, Mkoa KILIMANJARO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 04/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SEFU SALIMU MSOFE WA LEMBENI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MWANAIDI RAMADHANI MSOFE**

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imtolewa leo tarehe 06/06/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABEID OMARY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0661/0038** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **ISENYE mwaka 2010**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DOM/UDOM/RB/930/2016**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VERONICA KANGWA** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kuhitimu Shahada ya Kwanza – Science in Insurance and Risk Management chenye namba **BIR/11/49711** kilichotolewa na Institute of Finance Management (IFM) mwaka **2015**.

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi,

**Taarifa polisi: DAR/CHU/RB/107962/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SECILIA THOMAS MLAMBALAMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2053-0049** kilichotolewa na Baraza la mitihani la taifa kupitia **CHITA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/309326/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAULO ROBERT SWEYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 389 AUM** aina ya **MITSUBISH-FUSO** yenye jina la **TACHI ENTERPRISES,** Chasis No. **FK618E2520077,** Engine No. **6D17867087.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NY/RB/235402/2022**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**DAVID MIBAROY MOLLEL** anatangaza kupotelewa na passport ya kusafiria yenye namba **AB490556** iliyotolewa Dar Es Salaam na wizara ya mambo ndani ya nchi **UHAMIAJI** mwaka **2011**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa ARU/ARU/RB/235548/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RICHARD MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye **USAJILI NAMBA T165 BSF, CHASSIS NAMBA: KFKE700007741, ENGINE NAMBA: 162FMJPK028300.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/AR/RB/236884/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ..........TANGA............**
**Kituo cha ...MJINI- TANGA .... Mkoa.....TANGA.........**
**Shauri la Ndoa Na..............28/2022.........**
**Jina la mdai....ZERA WILLIAM OWINO.........**
**Jina la Mdaiwa: ...MORIS ODONGO OMING'O.........**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa ... MORIS ODONGO OMING'O .................**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ya .........**TALAKA, MGAWANYO WA MALI ZA NDOA NA MATUNZO YA WATOTO**........................

kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii 23/6/2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta ushahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaweza kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo 9/06/2022

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**ALLY SAID ALLY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.2823/0029** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GOROWA SEKONDARI** mwaka 2016. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/236277/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **HOSSEA ENOCK MAKOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **MC 495 CVU.** Yenye Engine namba **157FM1220F02191** na Chassis namba **LDAPAKOB4LGB03711.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa Polisi: MUH/RB/1732.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN FANUEL MAKALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA STARLET** yenye USAJILI NAMBA: **T512 AMF**, CHASSIS NAMBA: **EP950006985**, ENGINE NAMBA: **4E1793870**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/237491/2022**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mahakama yasitisha uhamishaji wa wahamiaji

**LONDON,** Uingereza

UINGEREZA imesema ina imani kuwa inaweza kushinda vizingiti vyovyote vya kisheria vya kuizuia serikali kuwaondoa watu wanaotafuta hifadhi nchini humo.

Hatua hiyo inatokana na uamuzi wa dakika za mwisho kutoka kwa majaji wa Mahakama ya Ulaya inayoshughulikia Haki za Binadamu (ECHR) ambayo jana ilizuia safari ya ndege ya kwanza iliyokuwa imewabeba wahamiaji kuwapeleka nchini Rwanda.

Serikali ya Uingereza imelazimika kukabiliana na mfululizo wa kesi zilizofunguliwa katika mahakama mbalimbali mjini London kupinga kuondolewa kwa wahamiaji hao.

Mashirika ya misaada, wanasiasa na viongozi wa kidini wameishtumu serikali ya Uingereza kwa kuendesha vita visivyozingatia haki za binadamu dhidi ya watu wanaoomba hifadhi nchini humo.

Hata hivyo, serikali ilijitetea kwa kusema inawaondoa wahamiaji hao ili kuzuia biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Waziri wa Ajira, Therese Coffe (pichani chini) aliliambia shirika la habari la Sky News, kuwa serikali ilikuwa inajiandaa kuwasafirisha kwa ndege wahamiaji hao hadi Rwanda.

Hata hivyo, Waziri huyo alisema watakata rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama ya ECHR iliyoizuia Uingereza kuwaondoa wahamiaji hao

Hata hivyo, Rwanda ilisema jana kuwa haijakata tamaa baada ya safari ya kwanza ya ndege iliyopaswa kuchukua waomba hifadhi kutoka Uingereza kuwapeleka nchini humo kuahirishwa.

Safari hiyo ya ndege ilisitishwa baada ya uingiliaji kati wa Mahakama ya Ulaya ya Haki za Kibinadamu (ECHR) na kusababisha changamoto mpya katika mahakama za Uingereza.

"Hatukatishwi tamaa na yaliyojiri, Rwanda inasalia kujitolea kikamilifu kufanya ushirikiano huu ufanye kazi. Hali ya sasa ya watu wanaofanya safari za hatari haiwezi kuendelea kwani inasababisha mateso yasiyoelezeka kwa wengi," alisema msemaji wa serikali ya Rwanda, Yolande Makolo. **DW**



# Zelensky akiri kupata hasara kubwa, miji muhimu kutekwa

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amekiri vikosi vyake vimepata hasara kubwa kwenye mapigano yanayoendelea katika mji wa Severodonestsk na mkoa wa Kharkiv.

Katika hotuba yake ya usiku wa manane wa jana, Rais Zelenskiy, alisema Ukraine inahitaji silaha za kisasa za kuzuia makombora ili kujilinda.

Alisema hakuna sababu ya msingi kwa mataifa washirika kuchelewesha uwasilishaji wa silaha hizo.

Alikiri kwamba makombora ya Russia yanakwepa mifumo ya ulinzi na kusababisha vifo.

Hata hivyo, alisema vikosi vyake vinajaribu kuwaondoa raia kutoka mji wa Severodonetsk baada ya Russia kuharibu daraja la mwisho kuingia mjini humo.

Kwa upande mwingine, Russia ilisema imefungua njia ya kiutu kutoka kiwanda cha kemikali ya ammonia kilichoasisiwa chini ya utawala wa kiongozi wa Kisovieti Josef Stalin, kwenda mjini unaodhibitiwa na wanaotaka kujitenga.

Ofisa wa juu nchini Ukraine alisema mapigano mjini Severodonestsk na maeneo mengine mashariki mwa nchi hiyo yanazidi kuwa magumu, lakini wanajeshi wake wamemzuia adui kwenye pande nyingine tatu kwa wakati mmoja.

Zelenskiy ameyataka mataifa ya magharibi kuipatia Ukraine mifumo ya kisasa zaidi ya kuzuia makombora.

Gavana wa Luhansk, Serhii Haidai alisema kupitia mtandao wa kijamii wa Telegram, kwamba vita hiyo imezidi kuwa ngumu kwa jeshi la Ukraine, lakini akaongeza kuwa vikosi vyake vinaendelea kuilinda Severodonetsk na haviruhusu kusonga mbele kuelekea Lysychansk.

> **Lakini ni sehemu tu ya makombora tuliyoweza kuangusha. Kwa bahati mbaya tuna majeruhi na uharibifu. Katika mikoa ya Lviv na Ternopil ilipigwa.**

Kulingana na Haidai, kuna watu wengi waliojeruhiwa katika mji wa Lysychansk, unaotenganishwa na mto na Severodonetsk.

Vikosi vya Russia vinajaribu kupunguza upinzani wa Ukraine katika mji huo wa mashariki, katika juhudi zao za kuwaondoa wanajeshi wa serikali kutoka mikoa miwili ya waasi wanaotaka kujitenga ambayo nchi hiyo inaiunga mkono.

Vita katika mji wa Severodonetsk, ambao ni mji wenye wakazi 100,000, hivi sasa ndiyo kitovu cha mapigano makali zaidi nchini humo.

Akizungumzia uhitaji wa mifumo ya kujilinda, Rais Zelensky, alisema baadhi ya maroketi ya Russia yanakwepa mifumo ya ulinzi na kusababisha maafa makubwa.

"Lakini ni sehemu tu ya makombora tuliyoweza kuangusha. Kwa bahati mbaya tuna majeruhi na uharibifu. Katika mikoa ya Lviv na Ternopil ilipigwa," " alisema.

Aliongeza "Nchi yetu haina silaha hizo kwa kiwango cha kutosha wakati mahitaji ya aina hiyo ya silaha ni makubwa. Ucheleweshaji wa kutoa silaha hauna kisingizio."

Kiongozi huyo aliyasihi mataifa hayo ya magharibi kuharakisha utoaji wa silaha kwa nchi yake.

Hata hivyo, katika taarifa fupi zilizotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Russia, ilidai vikosi vyake vimefanikiwa kuharibu ghala la silaha zilizotolewa na jumuiya ya NATO, kwa ajili ya Ukraine karibu na mji wa Zolochiv katika mkoa wa Lviv.

**NATO KUENDELEA KUTOA SILAHA**

Katibu Mkuu wa Muungano wa Nato, Jenerali Jens Stoltenberg, aliwaambia waandishi wa habari kwamba Ukraine iko katika hali mbaya na kuna haja ya kupewa msaada wa dharura.

Stoltenberg alisema wajumbe wa muungano huo wataendelea kuipatia Ukraine silaha nzito na mifumo ya masafa marefu na alisisitiza anatarajia awamu mpya ya msaada kwa nchi hiyo itakubaliwa katika kikao cha Nato.

"Tunalenga kabisa kuingilia kati na kusaidia , alisema Stoltenberg. **DW**



Moshi ukitanda kila kona ya mji wa Severodonetsky ambao umekuwa kiini cha mapigano kati ya vikosi vya Russia na Ukraine jana. **PICHA REUTERS**

# Gharama ya mafuta Kenya yazidi kupaa

**NAIROBI,** Kenya

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Petroli nchini Kenya (Epra) imetangaza kupanda kwa bei ya mafuta kwa shilingi tisa katika upangaji wake wa bei kwa kila mwezi.

Kwa muda wa mwezi mmoja ujao, lita moja ya petroli jijini Nairobi itagharimu Shilingi 159.12, dizeli 140 na mafuta taa 127.94.

Epra ilisema katika taarifa yake kwamba serikali itatumia Hazina ya Maendeleo ya Petroli (PDL) kuwaepusha watumiaji kupanda kwa bei hiyo.

Huku madereva wa vyombo vya moto jijini Nairobi wakilipa Sh.159.12 kwa lita moja ya petroli, lakini bei halisi ilikuwa Sh184.68, kama serikali isingeweka ruzuku ya Sh25.76 kwa lita.

Epra ilisema bei hizo zinajumuisha kodi na zimerekebishwa kulingana na mfumuko wa bei. **BBC**

# AZAM FC YAKANUSHA KUTETA USAJILI NA MKANDALA, MPOLE

**Na Saada Akida**

WAKATI Azam FC ikihusishwa kuwa katika mazungumzo ya usajili wa wachezaji kadhaa, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema mchakato huo kwa upande wao haujaanza ingawa mikakati yao ni kukiimarisha kikosi kwa kukijenga kuwa cha ushindani zaidi msimu ujao.

Majina ya wachezaji yanayotajwa kuwa tayari Azam imekamilisha mazungumzo nao ni kiungo wa Dodoma Jiji FC, Cleophace Mkandala, mshambuliaji wa Geita Gold, George Mpole huku wakiendelea kuzungumza na makipa, Justin Ndikumana na Onesime Rukundo kutoka timu ya Taifa ya Burundi pamoja na Mtenja Albano wa Coastal Union.

**Hata hivyo, licha ya Popat kuwakana, Nipashe lina taarifa za uhakika, kwamba viongozi wa Azam FC wako katika hatua nzuri za kukamilisha mazungumzo kati ya makipa hao na mmoja wapo huenda atasaini mkataba wa kuitumikia timu hiyo kwa msimu ujao.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Popat alisema hakuna mazungumzo yaliyofanywa na mchezaji yeyote hadi hapo watakapomaliza ligi, lakini matarajio yao makubwa ni kuhakikisha wanafanya usajili imara kuboresha kikosi chao.

Alisema kwa sasa wanapambana kwanza katika michezo mitatu iliyosalia kuhakikisha wanashinda mechi hizo ili kupata nafasi ya kuiwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa.

"Kwa sasa suala la usajili kwa upande wetu ni bado, kwa sababu dirisha halijafunguliwa na tuko katika mapambano ya kuhakikisha tunashinda hizi mechi tatu zilizosalia, lakini matarajio yetu makubwa ni kufanya usajili mkubwa kwa kuleta wachezaji wa ushindani," alisema Popat.

Alisema msimu huu hawakufikia malengo yao ikiwamo kutwaa mataji yote mawili na sasa wanahitaji kupambana ili kushinda mechi zilizosalia kujiweka katika mazingira mazuri ya kwenda kuwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa msimu ujao.




Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kushoto) akimkabidhi jezi na mpira Mwenyekiti wa timu ya Waandishi wa Habari za Michezo nchini (Taswa SC), Majuto Omary. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *M-Bet yaipiga tafu Taswa SC*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha nchini, M-Bet Tanzania, imesaidia vifaa vya michezo timu ya Waandishi wa Habari za Michezo nchini, Taswa SC, kwa ajili kutumika katika shughuli mbalimbali za michezo.

Vifaa hivyo ni jezi na mpira ambapo meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, amesema wamefikia hatua hiyo baada ya kuvutiwa na mwenendo wa Taswa SC katika mechi zake mbalimbali.

Taswa SC inatarajia kucheza mechi ya kirafiki na timu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Bunge SC), Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. Mbali ya mechi hiyo, timu ya Netiboli ya Bunge (Bunge Queens) nayo itapambana na Taswa Queens.

Kwa mujibu wa Mushi, M-Bet Tanzania inajisikia fahari kubwa kuisaidia Taswa SC katika shughuli zake na hasa katika mchezo wao wa Jumamosi.

"Ni faraja na fahari kubwa kuisaidia timu ya Taswa SC ili kufanikisha kucheza mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na msisimko mkubwa na ushindani pia. M-Bet itaendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za michezo na sekta nyingine ili kusaidia ustawi wake," alisema Mushi.

Mwenyekiti wa Taswa SC, Majuto Omary, aliipongeza Kampuni ya M-Bet Tanzania kwa kuwasaidia na kuwaahidi kutowaangusha katika mechi hiyo na nyinginezo zitakazofuata.

Majuto alisema bado wanachangamoto nyingi, lakini kutokana na mshikamano baina yao, wameweza kuzikabili na kusonga mbele.

"Huu ni msaada mkubwa sana kwetu na utafungua njia kwa makampuni mengine kutusaidia. Klabu ina mahitaji mengi na tunaamini taasisi, kampuni na watu binafsi watatusaidia," alisema Majuto.

## Hitimana aanika zakushuka daraja

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema kulingana na msimamo wa Ligi Kuu ulivyo kwa sasa, anaamini Simba na Yanga ndio timu pekee zenye uhakika wa kuendelea kubaki katika heka heka za Ligi Kuu msimu ujao.

Kauli hiyo ya Hitimana imekuja baada ya KMC FC kulazimisha sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema kuanzia nafasi tatu hadi ya mwisho hakuna mwenye uhakika wa kubaki Ligi Kuu, hivyo kilichopo ni kila timu kuendelea kupambana kuhakikisha inapata nafasi ya kujinusuru ili kubaki ligi hiyo msimu ujao.

Alisema KMC kuwa nafasi ya tisa kwa pointi 31, hawako katika hali mbaya pekee yao, bali kila timu iko kwenye hatihati ya kushuka daraja kuanzia nafasi ya tatu.

"Ukiangalia msimamo anayeshika nafasi ya tatu (Geita Gold yeye pointi 39), huku aliyepo nafasi ya nne (Namungo FC) na ya tano Azam FC wote wana pointi 37, kuanzia nafasi ya sita hadi ya chini tumepishana pointi tatu hadi nne," alisema Hitimana.

Alisema ligi imekuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya pointi chache zilizopishana kwa timu inayoshika nafasi ya tatu, anayefungwa anashuka na anashinda hupanda juu.

## Kagera na sababu sare na Biashara

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema mapumziko ambayo wachezaji wake waliyapata, yamewafanya kuwa waoga na ndicho kilichosababisha kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Biashara United juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Baraza alisema hakufurahishwa na suluhu hiyo kwa sababu nyingi, kwani walikuwa wanacheza nyumbani mbele ya mashabiki wao.

"Kuna uzembe umeingia kwa wachezaji wangu, walikwenda kupumzika kutokana na haya mapumziko ya Kalenda ya FIFA, lakini walipumzika kupitiliza kiasi kwamba hata waliporejea wakawa waoga, unaona hata kuanza mpira wanaogopa, kumfuata mpinzani wanaingiwa na woga, kifupi walikuwa hata mpira wenyewe hawautaki," alisema Baraza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imepeleka ofa ya kumsajili kiungo wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30, wakati huu mkataba wake na Brentford ukimalizika mwishoni mwa mwezi huu. ***(Athletic)***

### BAYERN BADO IPO NA MANE

KLABU YA Bayern Munich inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 34.6 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, hiyo ni baada ya Liverpool kukataa ofa mbili za awali za miamba hiyo ya Ujerumani. ***(Bild, via Mail)***

### POGBA AKARIBIA PSG

JUVENTUS inakaribia kumalizana na kiungo Mfaransa aliyeaga Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29. ***(Fabrizio Romano)***

### CITY KUINGIZA MILIONI 200

KLABU ya Manchester City inaweza kupata zaidi ya pauni milioni 200 kwa kuuza wachezaji msimu huu wakati klabu hiyo ikataka kumsajili kiungo wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26. ***(Telegraph)***

### RICHARLISON AIKATAA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Everton, Richarlison mwenye umri wa miaka 25, amekataa ofa ya kujiunga na Arsenal msimu huu - huku Chelsea na Tottenham Hotspur zikitajwa kama timu anazotaka kutua Mbrazil huyo. ***(UOL, via Liverpool Echo)***

### LUKAKU ANUKIA INTER

INTER Milan inapambana kumsajili Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kutoka Chelsea, na mshambuliaji huyo wa Ubelgiji anajiandaa kukubali mshahara kiduchu ili kurejea Seeia A. ***(Fabrizio Romano)***

### DE JONG KUNG'OLEWA BARCA

NIA ya Manchester United ya kumtaka Christian Eriksen haitabadilisha mbio zao kwa chaguo lao la kwanza Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, mazungumzo yanaendelea kufanyika na klabu ya kiungo huyo Mholanzi, Barcelona. ***(Mail)***

### OSIMHEN KUAMUA HATIMA

NYOTA anayehusishwa na Arsenal, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23, amesema ataamua hatima yake hivi karibuni baada ya nyota huyu wa Nigeria na Napoli kukiri kwamba, anasakwa na klabu kadhaa za England na Hispania. ***(Standard)***

### STRAKOSHA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanafikiria kumnunua mlinda mlango wa kimataifa wa Lazio na Albania, Thomas Strakosha mwenye umri wa miaka 27, ikiwa kipa wa Hispania, Kepa mwenye miaka 27 ataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### RAPHINHA NA ARSENAL, SPURS

WINGA wa Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, anasakwa na klabu za Arsenal na Tottenham Hotspur msimu huu wa majira ya joto, huku kukiwa na wasiwasi kwamba, Barcelona hawataweza kumsajii Mbrazil huyo. ***(Athletics)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# CHRISTENSEN: KILA MCHEZAJI ANATAMANI KUCHEZA BARCA

**Ni moja ya klabu kubwa barani Ulaya, iwapo wamekuwa na matatizo yao au la, bado ni...**

**LONDON,** England

ANDREAS Christensen anatumaini hivi karibuni atatangaza klabu yake ijayo baada ya kuondoka Chelsea, huku raia huyo wa Denmark akichochea uvumi kwamba, atajiunga na Barcelona kwa kuwataja kuwa moja ya klabu kubwa barani Ulaya.

**Chelsea ilitangaza kuondoka kwa Christensen wiki iliyopita, huku beki huyo akihusishwa sana na Barca.**

Christensen alijiunga na Chelsea kutoka Brondby mwaka 2012 na baada ya kudumu kwa mkopo kule Borussia Monchengladbach, akajiunga na 'Blues' ambapo amecheza mechi 161, akishinda Ligi ya Europa, Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup na Klabu Bingwa Dunia wakati akiwa Stamford Bridge.

Akiwa amecheza dakika zote 90 wakati Denmark iliposhinda 2-0 kwenye Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Austria Jumatatu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anatarajia kutangaza wapi atakapocheza hivi karibuni.

"Ninajua mahali ninapopaswa kucheza," alisema beki huyo akiwaambia waandishi wa habari.

Alipoulizwa wapi ataelekea, alijibu: "Kwa bahati mbaya, si juu yangu kabisa. Pia kuna mambo mengine ambayo yanapaswa kutekelezwa.

"Natumaini hivi karibuni. Lakini najua ninachokwenda kufanya. Nasubiri muda mwafaka."

Barcelona wamekumbwa na matatizo ya kifedha katika miaka ya hivi karibuni, huku rais wa LaLiga, Javier Tebas majuzi akisema timu hiyo inayonolewa na kocha Xavi lazima iuze mali ya thamani - kama kiungo wa kati Frenkie de Jong - ili kufadhili ujenzi wowote wa kikosi chao wakati wa dirisha la usajili.

Hata hivyo, Christensen, ambaye amekuwa akipigiwa upatu kutoa ushindani kwa mabeki wa kati wa sasa wa Barca, Gerard Pique na Ronald Araujo, amesema Barca ni timu ambayo inamvutia mchezaji yeyote.

"Ni moja ya klabu kubwa barani Ulaya," aliongeza. "Nadhani ni kwa kila mtu.

"Iwapo wamekuwa na matatizo yao au la, bado ni moja ya klabu kubwa kwa mchezaji kwenda kucheza."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,006,4

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
MBEYA CITY
1 | 1.31
X | 4.31
2 | 9.41

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED MAMBO MAGUMU KWA DE JONG



**MANCHESTER,** Uingereza

MANCHESTER United inahofia Barcelona wanajaribu kuongeza ada kwa Frenkie de Jong katika juhudi zao za kutaka kutatua matatizo yao ya kifedha, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu hizo mbili ziko kwenye mazungumzo ya kuuziana De Jong, ambaye ameipa United moyo wa kutosha kwamba, atakuwa tayari kuhamia Old Trafford chini ya kocha mpya, Erik ten Hag.

Kwa mujibu wa ESPN, Barcelona inataka kupata euro milioni 100, lakini United imepanga kutoa euro milioni 60 pamoja na nyongeza kidogo.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba hisia ndani ya klabu ni kwamba, Barca wanajaribu sana kumtoa De Jong katika juhudi za kutafuta fedha ili kuwezesha mipango yao ya kufanya usajili kipindi hiki cha majira ya joto. Ten Hag na Mkurugenzi wa Soka, John Murtough wanataka kwanza kununua kiungo wa kati kabla ya washambuliaji na mabeki, na De Jong ndiye anayepewa kipaumbele.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, awali alionekana kusita kuondoka Barcelona na kujiunga na klabu ambayo haipo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini msimamo huo umepungua.

Paris Saint-Germain pia walionyesha nia kutaka kumsajili De Jong, lakini kwa jinsi mambo yalivyo, United ndio chaguo linalofaa zaidi.



# *Matic aungana na Mourinh*

**ROME,** Italia

NEMAJA Matic ameungana na Jose Mourinho katika klabu ya AS Roma baada ya kuondoka Manchester United na kusajiliwa kwa uhamisho huru na timu hiyo ya Serie A.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amesaini mkataba wa mwaka mmoja kwa timu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Italia, akiungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa United, Henrikh Mkhitaryan na mwenzake wa zamani wa Chelsea, Tammy Abraham katika Uwanja wa Olimpico.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia, alithibitisha msimu uliopita kuwa utakuwa wa mwisho kwake pale Old Trafford, akiwa amekaa kwa miaka mitano Manchester, na amesajiliwa na Mourinho kwa mara ya tatu katika maisha yake ya soka.

"Nimefurahishwa na kuheshimiwa kujiunga na klabu hii na siwezi kusubiri kuanza msimu mpya na wachezaji wenzangu," alisema Matic akiwaambia waandishi wa habari.

"Roma ni klabu kubwa, yenye mashabiki wa ajabu na kocha, Jose Mourinho, ambaye anafahamika na kila mtu.

Mwaka 2014, baada ya miaka mitatu nchini Ureno, Matic alisajiliwa tena Ch wakati Mourinho alip kwa mara ya pili Stan Bridge, na miaka mitatu daye, alimfuata kocha wa Ureno pale Unite alikuwa akicheza mara mara katika kikosi cha k za kipindi chote cha uo wa Louis van Gaal na Gunnar Solskjaer.

United ililipa Chelsea ni milioni 40 kwa hud yake miaka mitano iliy na alicheza mechi 189 k mashindano yote akiw klabu hiyo, huku akiwa mu ya timu iliyomaliza washindi wa pili wa Kom FA msimu wa 2017-18 na ya Europa 2020- 21.

442,235/-

SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/06/22 | 20:00 | Enppi Club vs Coca Cola | 3.47 | 2.92 | 2.28 |
| 02. 18/06/22 | 21:30 | Gimnasia Mendoza vs Deportivo Maipu | 2.28 | 2.78 | 3.68 |
| 03. 18/06/22 | 22:00 | Londrina PR vs Vasco da Gama | 3.26 | 2.86 | 2.42 |
| 04. 18/06/22 | 22:00 | Seattle Sounders vs Los Angeles FC | 2.30 | 3.53 | 2.97 |
| 05. 19/06/22 | 00:00 | Arsenal Sarandi vs Talleres | 2.60 | 3.10 | 2.90 |
| 06. 19/06/22 | 00:30 | Nautico PE vs Sport Recife | 2.73 | 2.97 | 2.73 |
| 07. 19/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Ceara CE | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 08. 19/06/22 | 01:10 | Almirante Brown vs Deportivo Moron | 2.44 | 2.76 | 3.36 |
| 09. 19/06/22 | 01:45 | Sportivo Ameliano vs Nacional Asuncion | 2.77 | 3.12 | 2.57 |
| 10. 19/06/22 | 02:30 | Sarmiento vs Patronato Parana | 2.58 | 3.18 | 2.88 |
| 11. 19/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs DC United | 2.21 | 3.43 | 3.22 |
| 12. 19/06/22 | 13:30 | Suwon Samsung vs FC Seoul | 2.69 | 3.09 | 2.74 |
| 13. 19/06/22 | 17:00 | Guarani SP vs CSA AL | 2.42 | 2.97 | 3.12 |
| 14. 19/06/22 | 19:00 | Jerv vs Ham-Kam | 2.88 | 3.33 | 2.39 |
| 15. 19/06/22 | 21:00 | Aalesunds vs Valerenga | 2.46 | 3.39 | 2.74 |
| 16. 19/06/22 | 21:00 | Gimnasia Jujuy vs Temperley | 2.33 | 2.72 | 3.66 |
| 17. 19/06/22 | 22:00 | Tenerife vs Girona | 2.44 | 3.08 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 16/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1759 | AS Kigali vs Etoile de Lest | 1.95 | 3.63 | 3.19 |
| 13:30 | 2020 | Musanze vs Rutsiro FC | 5.10 | 3.09 | 1.72 |
| 14:30 | 1277 | Shandong Luneng vs Changchun Yatai | 1.94 | 3.30 | 3.55 |
| 14:30 | 2304 | Sichuan Jiuniu vs Shanghai Jiading Huilong | 1.26 | 4.91 | 9.83 |
| 16:00 | 1554 | Sebeta City FC vs Fasil Kenema | 9.85 | 4.73 | 1.27 |
| 16:00 | 2056 | Police FC Rwanda vs APR FC | 10.81 | 4.23 | 1.30 |
| 16:00 | 3161 | Kiyovu Sports vs Marines FC Gisenyi | 1.14 | 6.27 | 16.65 |
| 16:00 | 3580 | Namungo vs Polisi Tanzania | 2.17 | 2.70 | 3.73 |
| 17:00 | 1251 | Loko Tbilisi vs Saburtalo Tbilisi | 7.07 | 4.91 | 1.32 |
| 17:00 | 3144 | FC Gagra vs Dinamo Batumi | 6.48 | 4.81 | 1.36 |
| 17:00 | 4845 | FC Samgurali Tskaltubo vs Dinamo Tbilisi | 2.75 | 3.50 | 2.31 |
| 19:00 | 2956 | Simba vs Mbeya City | 1.31 | 4.31 | 9.41 |
| 19:00 | 3112 | Raja Casablanca vs Wydad Casablanca | 2.32 | 2.90 | 3.09 |
| 20:00 | 2608 | Vidar vs Sola | 1.48 | 4.70 | 5.20 |
| 20:00 | 3774 | IF Sylvia vs Motala Aif | 1.77 | 3.94 | 3.55 |
| 20:00 | 4802 | Torpedo Kutaisi vs Sioni Bolnisi | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 21:00 | 1853 | KA Akureyri vs Fram Reykjavik | 1.63 | 3.83 | 4.42 |
| 21:00 | 2721 | Thor Akureyri vs Grotta | 3.40 | 3.94 | 1.81 |
| 21:00 | 5069 | Augnablik vs Kari | 2.32 | 3.69 | 2.51 |
| 21:15 | 2992 | RS Berkane vs Difaa El Jadidi | 1.82 | 3.18 | 4.21 |
| 22:00 | 1768 | England W vs Belgium W | 1.15 | 6.30 | 13.78 |
| 22:00 | 2445 | Cruzeiro vs Ponte Preta | 1.39 | 3.88 | 8.05 |
| 22:00 | 3997 | Botafogo RJ vs Sao Paulo | 2.80 | 3.04 | 2.42 |
| 22:00 | 4740 | Audax Italiano vs San Antonio Unido | 1.24 | 5.29 | 9.40 |
| 22:15 | 1067 | Kordrengir vs UMF Selfoss | 1.87 | 3.69 | 3.40 |
| 22:15 | 1298 | Vaengir Jupiters vs Vidir | 2.80 | 4.23 | 1.98 |
| 22:15 | 2021 | Throttur Vogum vs Afturelding | 3.82 | 3.92 | 1.71 |
| 22:15 | 3062 | Reynir Sandgerdi vs Throttur Reykjavik | 6.26 | 5.29 | 1.33 |
| 22:15 | 4211 | Keflavik IF vs Stjarnan | 2.66 | 3.54 | 2.26 |
| 22:15 | 4711 | Hafnarfjordur vs Leiknir | 1.50 | 4.22 | 5.10 |
| 22:15 | 4866 | Fylkir vs HK Kopavogs | 1.93 | 3.73 | 3.19 |
| 22:15 | 5362 | UMF Grindavik vs KV Vesturbaer | 1.49 | 4.31 | 5.09 |
| 23:15 | 4025 | Valur vs Breidablik | 2.65 | 3.49 | 2.29 |
| 23:30 | 5458 | FAR Rabat vs Hassania Agadir | 1.86 | 3.18 | 4.02 |

IJUMAA - 17/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 2351 | Palmeiras vs Atletico GO | 1.33 | 4.60 | 7.63 |
| 00:00 | 3155 | Portuguesa FC vs Aragua FC | 2.14 | 2.85 | 3.54 |
| 01:00 | 2671 | Argentinos Juniors vs Independiente | 2.19 | 2.99 | 3.23 |
| 01:00 | 4987 | Avai vs Fortaleza CE | 2.99 | 3.04 | 2.29 |
| 01:00 | 5292 | Rosario Central vs Godoy Cruz | 2.47 | 3.21 | 2.61 |
| 02:00 | 1760 | Vila Nova GO vs Operario PR | 2.00 | 3.05 | 3.69 |
| 02:00 | 5285 | Alagoinhas AC BA vs Juazeirense | 2.13 | 2.95 | 3.44 |
| 02:15 | 4183 | Zamora FC vs Deportivo La Guaira | 1.97 | 3.24 | 3.54 |
| 03:00 | 2373 | Chicago FC United vs KAW Valley FC | 1.19 | 6.04 | 10.72 |
| 03:00 | 4620 | Chicago City SC vs FC Wichita | 1.17 | 6.45 | 10.76 |
| 03:30 | 1787 | Deportes Tolima vs Envigado FC | 1.27 | 4.61 | 10.79 |
| 03:30 | 3692 | Racing Club vs Velez Sarsfield | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 03:30 | 4399 | CA Platense vs Gimnasia y Esgrima | 2.85 | 3.05 | 2.38 |
| 03:30 | 5108 | La Equidad vs Independiente Medellin | 2.28 | 2.89 | 3.18 |
| 05:00 | 4542 | San Francisco City vs Project 51o | 5.40 | 4.10 | 1.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# PRISONS YANUSA HARUFU MBAYA KUSHUKA DARAJA

**Na Adam Fungamwango**

NI kama Prisons imenusa harufu ya kushuka daraja, baada ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Odhiambo, kusema kuanzia sasa ni lazima washinde mechi zilizobaki ili kujinusuru, la sivyo hawatopona.

Akizungumza juzi baada ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya KMC FC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kutoka sare ya bao 1-1, kocha huyo alisema sasa ni kufa ama kupona, na ili wasalie kwenye ligi hakuna kutoka sare zaidi ya ushindi.

"Nadhani kwa sasa ni lazima tushinde mechi zote tatu zilizobaki au hata mbili ili kujiweka kwenye mazingira mazuri, kwa hiyo lazima nikae na wachezaji, niongee nao na kuwaelekeza mazoezini mfumo ambao sasa utatuwezesha kucheza soka la kushambulia zaidi ili kupata ushindi. Ni ama tushinde au tufungwe basi, hakuna sare," alisema kocha huyo.

**Kwenye mechi hiyo alisema nia yake ilikuwa ni kupata pointi tatu na mipango yake ilikwenda vema hadi pale waliporuhusu bao, ndipo mfumo ulipobadilika.**

"Tulipanga kupata pointi tatu, tumekuja na mipango mizuri, lakini tukaruhusu bao, kwa hiyo tukabadili mfumo ili tupate angau pointi moja," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Thierry Hitimana, alisema wao walitambua mapema kuwa mechi hiyo ni ngumu, lakini kwa bahati mbaya sana wachezaji wake hawakucheza vizuri kwenye mchezo huo.

"Tuliwaambia mechi hii ni muhimu, sasa wachezaji wanaingiwa na presha kuliko Prisons wenyewe ambao walizihitaji zaidi pointi tatu kuliko sisi," alisema.

Kwa matokeo hayo, Prisons inakuwa kwenye nafasi ya 14 ikiwa na pointi 26, huku KMC ikishika nafasi ya tisa baada ya kukusanya alama 32.




Mshindi wa Jackpot Bonus ya SportPesa, Abasi Sudi Zuberi (45), akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.3 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Dulla Boys, Chuoni vita kupanda Ligi Kuu*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Dulla Boys na Chuoni FC, zimeendelea kuchuana vikali katika vita ya kuwania kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Dulla Boys katika mchezo wao wa juzi walishinda kwa mabao 4-1 dhidi ya Mwembe Makumbi FC wakati Chuoni wakiifunga Mchangani FC 3-0 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Mchangani.

Kwa matokeo hayo, Dulla Boys imefikisha alama 57 wakati Chuoni FC ikifikisha pointi 55 huku timu zote zikiwa zimebakiza mchezo mmoja kabla ya kuhitimisha ligi hiyo msimu huu.

Kwa matokeo hayo timu hizo zitasubiri matokeo ya mechi zao za mwisho kuamua itakayopanda daraja msimu huu kuungana na Kundemba FC wakati huu ambao Dulla Boys inapewa nafasi kubwa zaidi.

Dulla Boys inahitaji kushinda mchezo wake huo wa mwisho ili kupanda daraja na msimu ujao kucheza Ligi Kuu wakati Chuoni ili ipande daraja lazima ishinde mechi yake ya mwisho huku ikiombea mabaya Dulla Boys kufungwa au kutoka sare.

Kwa Upande wa timu zizoshuka daraja mpaka sasa, ni Mchangani FC, Bridge Star na Afrika Coast zimeaga rasmi ligi hiyo huku timu ya moja ikisubiriwa kuungana nazo.

Kati ya timu tatu, moja ambayo itafanya vibaya michezo miwili iliyobaki itashuka daraja ambazoo ni New Power yenye alama 30 katika nafasi ya 13, Kilimani City iliyopo nafasi ya 12 na pointi zake 30 pamoja na New King ambayo ina alama 33 katika nafasi ya 11.

# Michezo

Alhamisi Juni 16, 2022

Nipashe




Matic aungana na Mourinho Roma

UKURASA 22

KIMO...



Wachezaji wa Simba, Henoc Inonga 'Varane' (kulia) na John Bocco wakiwania mpira wakati wa mazoezi, timu hiyo itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam leo, kuikaribisha Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Matola azipania 3 za Mbeya City leo

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kwamba hawana cha kupoteza kwenye Ligi Kuu Bara kutokana na matumaini ya kutetea ubingwa wao kutoweka, Klabu ya Simba imesema leo inakwenda kulipa kisasi katika mchezo wao dhidi ya Mbeya City utakaopigwa usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ikumbukwe katika mchezo wa raundi ya kwanza ambao timu hizo zilikutana katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, wenyeji waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Klabu ya Simba, Selemani Matola, alisema lengo ni kushinda michezo yao yote iliyobaki kwani hakuna mchezo rahisi kwao msimu huu.

"Haijalishi kuwa hatuna cha kupoteza, tunataka pointi tatu kwenye mchezo huo, licha ya kwamba walitufunga nyumbani kwao katika mchezo uliopita," alisema Matola.

Kocha huyo alisema wamejiandaa vizuri kuelekea kwenye mchezo huo ambao utakuwa na ushindani na kudai hawawezi kukubali kufungwa mara mbili na wapinzani wao hao.

Alisema kiungo wao, Clatous Chama ameanza kufanya mazoezi mepesi mepesi pamoja na wachezaji wengine ambao walikuwa majeruhi na wanaendelea vizuri.

"Mpaka leo (jana) jioni, tutafahamu ni wachezaji gani ambao wataukosa mchezo huo baada ya kupata ripoti ya daktari wetu, tunawashukuru mashabiki wetu kwa ushirikiano wanaouonyesha katika kipindi chote hiki ambacho tunapata matokeo mabaya na mazuri," alisema Matola.

Alisema licha ya kuondoka aliyekuwa Kocha Mkuu, Pablo Franco, wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri. Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Antony Mwamlima, alisema wamejipanga vizuri kukutana na Simba inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC.

"Tumejipanga kukutana na Simba, tunaishehimu timu hiyo ina wachezaji wazuri hivyo tutaingia tukiwa na tahadhari kubwa," alisema Mwamlima.

# SIMBA REKODI NYUMBANI, YANGA MECHI ZA UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Geita Gold, Kagera Sugar nazo zatingisha huku Mbeya Kwanza ikipoteana zaidi kwa...

TIMU ya Simba imekuwa kinara wa kushinda mechi za nyumbani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku Yanga ikiwa inaongoza kwa kushinda ugenini hadi kufikia raundi ya 27 ya Ligi Kuu.

**Simba imecheza mechi 12 nyumbani, ikishinda mara 10 na kuwa timu pekee iliyoshinda mara nyingi zaidi.**

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, haijapoteza mechi yoyote ya nyumbani mpaka sasa, ikitoa sare mbili.

Kwenye mechi za ugenini, Yanga imecheza mechi 14, ikishinda 10 na sare nne, nayo haijapoteza mechi yoyote ya ugenini, na hata nyumbani.

Wakati Simba ikiongoza kwa kukusanya pointi 32 dhidi ya 30 za Yanga kwenye mechi za nyumbani, watani wao hao ugenini wamekusanya pointi 34.

Timu zote mbili zinafuatana, kwani kwenye mechi za nyumbani ambako Simba inaongoza, Yanga inashika nafasi ya pili kwa kucheza mechi 12, ukiondoa ya jana dhidi ya Coastal Union na imeshinda mechi tisa na kutoka sare tatu hivyo kuvuna pointi 30.

Simba inakamata nafasi ya pili kwa kushinda ugenini ambako Yanga inaongoza, ikiwa imecheza mechi 13, imeshinda nne, sare saba na kufungwa mechi mbili.

Timu ya Geita Gold inashika nafasi ya tatu kwa kufanya vizuri kwenye mechi zake za nyumbani, ikicheza mechi 12, kushinda saba, sare tatu na kupoteza mbili, ikipata pointi 24 kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Mbeya Kwanza ni timu ambayo haijautumia vema uwanja wake wa nyumbani, kwani imeshinda mechi tatu tu kati ya 13 ilizocheza, ikitoa sare tano na kupoteza tano pia, ikipata pointi 14.

Timu ya Kagera Sugar inashika nafasi ya tatu kwa kufanya vema kwenye mechi za ugenini, kwani kwenye mechi 14 ilizocheza, imeshinda nne, sare tano na kupoteza tano, ikikusanya pointi 17, huku timu iliyofanya vibaya zaidi kwenye mechi za nyumbani ni Prisons ikicheza 12, kushinda moja, sare nne na kupoteza mechi saba, ikikusanya pointi saba tu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042